epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumamosi Oktoba 12, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581827
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA WA 3
**Mtuhumiwa** wa wizi alivyojifanya muuza duka, anusurika kifo kwa kuchomwa moto



UKURASA WA 4
**Lukuvi** aeleza uzoefu wake vyama vingi



UKURASA WA 5
**Mwinyi** asema mafanikio utalii yameitangaza nchi kimataifa

UKURASA 22
**HAALAND AWEKA REKODI NORWAY**

# Samia ataka uchaguzi mitaa usitie doa taifa

• **Balozi** Nchimbi ataka CCM kutenda haki... *Ukurasa 2*




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akijiandikisha kwenye Daftari la Wapigakura kwa ajili ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika Kitongoji cha Sokoine, Chamwino mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**



UKURASA 21
**RONALDINHO AJIUNGA UMILIKI WA GREENVILLE**

## Dk. Mpango awa mbogo ubadhirifu wa bilioni 1.2/- za wakulima tumbaku

UKURASA 3



## JK asema Nyerere atakumbukwa kwa harakati za ukombozi Afrika

UKURASA 3

**MICHEZO** **MAXI: HAKUNA DABI RAHISI DUNIANI KOTE** UK.24 **KATUNI** UK.6



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, akijiandikisha katika Daftari la Wakazi kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa katika Ofisi ya Serikali ya Mtaa wa Masaki, Kata ya Msasani Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Rais Samia ataka uchaguzi wa Serikali Mitaa usitie doa taifa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan amewataka Watanzania kuhakikisha uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajia kufanyika mwezi ujao, unamalizika salama bila kulitia doa taifa kwa kuwa ndio utakaoonesha taswira ya uchaguzi mkuu mwakani.

Amesisitiza umuhimu wa kuchagua viongozi wa ngazi ya serikali za mitaa na kueleza kuwa hata yeye anapokwama katika masuala yanayohitaji idhini ya Mwenyekiti wa Mtaa wake, humfuata mtaani.

Akizungumza jana baada ya kujiandikisha katika Daftari la Mpigakura Serikali za Mitaa katika Kitongoji cha Sokoine, wilayani Chamwino, mkoani hapa, Rais Samia alisema ni muhimu kila Mtanzania kudumisha amani na usalama katika uchaguzi huo bila kulitia doa taifa.

"Niwaombe sana mchakato ufanyike kwa usalama na kwa amani ili tusiitie doa nchi yetu, tumalize uchaguzi wa awali salama. Mchakato huu utatoa taswira ya uchaguzi mkuu ujao. Niwaombe wananchi tujitokeze tukachague vyema ili tupate sura halisi mbele tunakokwenda," alisisitiza.

Rais Samia alisema kwa kuwa uchaguzi huo utafanyika siku ya Jumatano, itatangazwa baadaye wananchi wasiende kazini ili kushiriki kupiga kura.

"Kumekuwapo na mkanganyiko kati ya daftari hili na daftari la Tume Huru ya Uchaguzi. Haya ni madaftari tofauti, hivyo wananchi wajitokeze kwa wingi kujiandikisha na kushiriki kuchagua viongozi bora watakaowaongoza katika maeneo yao.

"Kuna ubabaifu unajitokeza wengine wanahisi akishajiandikisha kwenye daftari lile la Tume ya Uhuru ya Uchaguzi, hana haja ya kujiandikisha huku hapana.

"Tunajiandikisha kule kwa uchaguzi wa mwakani lakini hapa kwenye eneo lako unachagua mwenyekiti wako wa kitongoji na kamati yake na viongozi wengine. Ni daftari lingine tofauti, kwa hiyo niwaombe wote kuanzia leo (jana) hadi Oktoba 20 mwaka huu, kila mmoja kwa nafasi yake ajitokeze kujiandikisha," alisisitiza.

Kuhusu umuhimu wa uchaguzi huo, Rais Samia alisema viongozi watakaowachagua ndio watasaidia kuweka usalama na amani katika maeneo yao.

"Katika utambuzi wa watu kwenye maeneo yetu ni dhamana yao nani kaingia, nani katoka, nani anashughuri gani, nani hana, kesi ndogo ndogo wao wanaweka usalama wa maeneo yetu lakini kubwa la utambuzi," alisema.

Rais Samia alisema kila mwananchi mwenye mahitaji mbalimbali katika eneo lake kuanzia kwa viongozi hao hata yeye amekuwa akienda kwa mwenyekiti wake.

"Hata mimi mbali na makuta (kuta) yale (Ikulu) kuna shida nyingine ni kijaza fomu ninaulizwa mwenyekiti wangu wa kijiji ni lazima nitoke kwenye makuta (yale), nimfuate nipate idhini yake na muhuri wake ili kupata huduma nyingine. Sasa jiulize usipokwenda kumchagua, ukachaguliwa ukawekewa ambaye hukudhania utawekewa.

"Tunapofanya shughuli zote za maendeleo hawa ndio wa kwanza katika maeneo yao tunawasukuma watoe watu washiriki, sasa akiwa mzembe utaanza kulalamika kiongozi mwenyewe ni mzembe, lakini hukwenda kumchagua. Ukienda kumchagua wewe na wenzako mtaweka mtu anayefaa kuwatumikia," alisisitiza.

Rais Samia alisema uchaguzi huo ni uhuru wa demokrasia na tamaduni ambapo Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka mfumo wa tawala za mikoa.

"Usiposhiriki unakiuka Katiba inayokuongoza ndani ya nchi yako, mfumo huu ni mfumo wa kikatiba na ni haki kwa kila mtu kushiriki kuchagua au kuchaguliwa.

"Kila anayeanzia miaka 21 mkimwona mzuri wa jinsia yoyote, anajituma, anasifa, anamwingiliano mzuri na watu na yupo mbele katika shughuli za maendeleo akijitokeza kuomba kuchaguliwa, basi mchagueni. Mmemwona anafaa lakini yupo nyuma hataki kwenda anaogopa kushindwa na mnahakikisha huyu mzuri atatusaidia msukumeni, mwambieni hebu nenda chukua fomu.

"Huu mchakato ni kila mwenye sifa anaomba tunachujana vizuri bila kupendeleana na wale wazuri tunaowaona hawa watatuongoza vizuri, basi tunawapeleka wakashindane na mmoja wao akiibuka ndio kiongozi wetu," alisema.

## ... Balozi Nchimbi ataka haki itendeke

**Na Halfani Chusi,** KAHAMA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, amewataka viongozi wa CCM kutenda haki kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, unaotarajia kufanyika mwezi ujao.

Balozi Nchimbi aliyasema hayo jana wilayani hapa ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kikazi ya siku tatu mkoani Shinyanga, akiambatana na Katibu wa NEC - Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla na Katibu wa NEC - Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, Rabia Hamid Abdalla.

Alisema kila mwanachama wa CCM ana haki sawa na mwingine, akisisitiza kuwa ni kinyume cha maadili ya chama hicho kumnyima mtu mwenye sifa nafasi ya uongozi kutokana na chuki binafsi.

"Tunakoelekea katika uchaguzi utekelezaji wa haki unatakiwa. Acheni kupanga safu. Viongozi bora ndio wapitishwe ni kosa kubwa la kimaadili ndani ya CCM kiongozi kumkamia mwanachama.

"Kwamba eti safari hii nitahakikisha fulani anakatwa katika chama chetu. Hiyo hapana, kwani kila mwanachama ndani ana haki sawa na mwingine. Tuna watu, ukimalizika uchaguzi ndani ya chama chetu, mnaanza upelelezi nani ambaye hajamuunga mkono na kuanza kumshughulikia. Hiyo ni tabia mbaya na haikubaliki.

"Mtu kukupigia kura ni haki yake na anapokunyima kura ni haki yake pia. Kuna viongozi wengine wamejigeuza kuwa miungu watu, hiyo hapana, viongozi wazuri husambaza upendo," alisema.

Balozi Nchimbi alimpigia simu Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, kuhusu ombi la Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, linalohusu Kahama kuwa mkoa wa ki- TANESCO.

Katika majibu yake, Dk. Biteko alikiri kwamba walipokea maombi ya mbunge na tayari wameshafanya uchambuzi kwenye maeneo ambayo wanaanzisha mikoa ya ki-TANESCO.

"Kwa Kahama ni mkoa ambao kwanza utajengwa mtambo mkubwa wa kusafisha ambao utafanya uchenjuaji wa madini ya Kabanga na maeneo mengine kwa hiyo kutahitajika umeme mwingi.

"Pili, Kahama kuna mgodi mkubwa wa Bullyanhulu ambao unaipatia (serikali) mapato mengi na baada ya kufanya uchambuzi tumejiridhisha pamoja na kilimo cha tumbaku kinachofanyika upande wa Ushetu na maeneo mengine, tumeona ni muhimu kusogeza huduma kwa wananchi kwa sababu wanahitaji umeme," alisema.

Dk. Biteko alisema katika mwaka huu wa fedha wanatarajia kukamilisha uchambuzi ili Kahama kuwa mkoa wa ki-TANESCO. Naye Makalla alitoa wito kwa Watanzania na wanachama wa CCM kujiandikisha katika Daftari la Makazi ili kuhakikisha wanapata fursa ya kupiga kura katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika mwezi ujao.

Alisisitiza kuwa mchakato huo ni muhimu kwa kila mwananchi anayependa kushiriki katika kuchagua viongozi watakaoleta maendeleo ya haraka katika maeneo yao. Makalla aliwataka mabalozi wa CCM kote nchini kuwahamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi kujiandikisha.

Alisisitiza kwamba ili maendeleo yafikiwe kwa haraka, ni muhimu kuchagua viongozi wenye weledi na maono ya maendeleo. Rabia Abdalla, alisisitiza umuhimu wa mshikamano na upendo miongoni mwa viongozi na wanachama wa CCM. Alisema viongozi wanapaswa kuwa mfano mzuri wa kuigwa katika kuonesha upendo, umoja na mshikamano na kwamba, hayo ni maadili muhimu kwa kiongozi yeyote anayejali maslahi ya wananchi.

Rabia alisema chama hicho kitatilia mkazo maadili hayo katika kuhakikisha kuwa viongozi wake wanatimiza wajibu wao kwa ufanisi.

## Mtuhumiwa wa wizi alivyojifanya muuza duka, anusurika kifo

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Kata ya Rasbura, Manispaa ya Lindi, mkoani hapa, Juma Kiona (21), anayetuhumiwa ni kibaka, amenusurika kifo kwa kuchomwa moto baada ya kufika katika duka la mtu na kujigeuza muuzaji kwa lengo la kuiba.

Kiona ambaye amelazwa Hospitali ya Sokoine, mkoani humo anauguza majeraha aliyoyapata baada ya wananchi kumshtukia na kumchoma moto.

Majirani katika duka kulikofanyika tukio hilo lililoko Mtaa wa Mitema Katani, walisema mtuhumiwa huyo alichomwa moto Jumatano ya wiki hii majira ya mchana.

Wakisimulia mkasa huo kwa nyakati tofauti, Gabriel John, Sofia Yusufu na Ashura Hemed walisema mtuhumiwa huyo alifika nyumbani kwa mwenye duka, maarufu kama Mama Mkunguru, na kuingia dukani kisha kufungua droo ya kuhifadhia fedha kwa lengo la kuzichukua.

"Alipata mwanya huo kutokana na mwenye duka wakati huo alikuwa ametoka kwenda ukumbini," alisema.

Akizungumzia tukio hilo Mama Mkunguru, alisema mtuhumiwa huyo alipata upenyo wa kuingia dukani kwake wakati yeye akiwa varandani akila chakula.

"Nikiwa varandani na watoto wangu huyu kijana aliingia dukani kupitia mlango mdogo wa nje na kuanza kuchukua fedha kutoka ndani ya droo," alisema.

Alisema wakati wakiendelea kula walisikia sauti ya droo analotumia kuweka fedha dukani humo kama linafunguliwa na alipokwenda alikuta mtuhumiwa huyo amejigeuza muuzaji anawahudumia wateja waliokuwapo hapo wakati huo wakitaka huduma.

Alisema baada ya kufika mtuhumiwa huyo alitimua mbio ndipo wateja waliokuwapo eneo hilo wakapiga kelele za mwizi na kukamatwa na ndipo alipochomwa moto.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Mkoa wa Lindi ya Sokoine, Dk. Alexander Makalla, alikiri kumpokea mtuhumiwa huyo aliyefikishwa hospitalini hapo na askari wa Jeshi la Polisi akiwa na majeraha maeneo mbalimbali ya mwili wake.

Dk. Makalla alisema Kinona ameungua moto maeneo ya mgongoni, mikononi na miguuni na hali yake inaendelea vizuri.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Kamishna Msaidizi (ACP) John Imori, alikiri kufahamu tukio hilo na kuwataka wananchi kuacha tabia ya kujichukulia sheria mikononi pindi wanapomkamata mhalifu badala yake wafuate sheria.

# JK asema Nyerere atakumbukwa kwa harakati za ukombozi Afrika

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

RAIS Mstaafu Jakaya Kikwete amesema nchi za Afrika zitamkumbuka Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, kama kinara wa kupambana na ukoloni na kuwaunganisha Waafrika kuwa kitu kimoja.

Kikwete alisema hayo jana alipongoza mdahalo wa Kumbukizi ya Mwalimu Julius Nyerere ambao ulijikita kuzungumzia harakati alizozifanya kipindi cha uhai wake.

Mdahalo huo uliofanyika katika Shule ya Uongozi ya Mwalimu Nyerere, Kwamfipa, Kibaha mkoani Pwani, ulizungumzia zaidi harakati za Ukombozi, Tafakuri ya Mshikamano wa Uongozi wa Afrika na Umoja wa Afrika.

Alisema Mwalimu Nyerere alihakikisha Tanganyika (kabla ya kuungana na Zanzibar na kuwa Tanzania) inapata uhuru wake. Kutokana na kujitoa kwake huko, alisema Nyerere atakumbukwa kwa mambo makubwa ambayo ameyafanya ambayo yanaendelea kuishi kwenye mioyo ya Watanzania na Afrika kwa ujumla.

Pia alisema nchi za Afrika zitamkumbuka Mwalimu Nyerere katika kuwa mstari wa mbele kuhakikisha Afrika yote inakuwa huru na mataifa yote yanaungana kutetea haki zao.

Alisema Nyerere alishirikiana na viongozi wa mataifa yaliyo Kusini mwa Afrika katika kuhakikisha nchi zote zinakuwa huru na kujitegemea. Kwa harakati hizo, lazima Waafrika wamuenzi na kumkumbuka.

"Alifanikisha vyama vya Kusini mwa Afrika kuungana na kushirikiana na China. Alikuwa mmoja wa watu waliofanikisha ushirikiano wa vyama sita vya ukombozi Kusini mwa Afrika Tanzania (CCM), Angola (MPLA), Namibia (SWAPO), Afrika Kusini (ANC), Zimbabwe (ZANU - PF) na Msumbiji (FRELIMO) na kushirikiana na Chama cha Kikumunisti cha China (CPC)," alisema.

Pia alisema Nyerere aliamini kuwa ili Waafrika wafanikiwe lazima nchi zote ziwe huru, hivyo ndiyo sababu ya kutaka kuzipigania nchi zote ili ziwe huru. Aliamini kwamba uhuru wa Tanzania hauwezi kuwa kamili mpaka Afrika nzime iwe imepata uhuru.

Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi, alisema Nyerere ni nuru ambayo inapaswa kuenziwa kutokana na alivyoongoza na kutamani kuona wananchi wanapata maendeleo.

Kabudi alisema mwalimu aliacha alama kwa kuwa alikuwa mmoja wa viongozi bora Afrika ambao wanapaswa kukumbukwa na kuenziwa kwa yale aliyoyafanya.

Naye Mkuu wa Shule ya Uongozi ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Prof. Marcelina Chijoriga, alisema kuwa wanaishukuru China kwa kujenga shule hiyo ambayo inaendeshwa na vyama sita vilivyopigania ukombozi wa kusini mwa Afrika ambayo ni matunda ya Nyerere.

Prof. Chijoriga alisema shule hiyo ni kumbukumbu nzuri ya kujifunza yale ambayo aliyafanya Nyerere kwa kuwa kuna mambo mengi ambayo yanafundishwa kutokana na yale aliyoyafanya mwasisi huyo ambaye ni nguli wa siasa Afrika na dunia.

Mdahalo huo ulihudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwamo mabalozi wa nchi sita zinazowakilisha nchi zenye vyama hivyo na wadau mbalimbali ambao wana historia ya Mwalimu Nyerere.




Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Mji Mpya, Kata ya Majohe, jijini Dar es Salaam, wakiandamana kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike, shuleni hapo, jana. Kushoto ni Msimamizi wa klabu za kupinga ukatili shuleni kutoka Kituo cha Taarifa na Maarifa Majohe, Halima Masoud. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mpango awa mbogo ubadhirifu bil.1.2/-

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ameshtushwa na tuhuma za ubadhirifu wa Sh. bilioni 1.2 za wakulima wa tumbaku katika Chama cha Ushirika cha Kisanga, Sikonge mkoani Tabora.

Kutokana na ubadhirifu huo, Dk. Mpango ameagiza Wizara ya Kilimo, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na taasisi zingine zinazohusika kuchukua hatua ikiwamo kuwasimamisha kazi wahusika wote.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Makamu wa Rais jana, Dk. Mpango alisema hayo wakati akizungumza na wananchi wa wilaya ya Sikonge katika mkutano wa hadhara uliofanyika viwanja vya TASAF akiwa ziarani mkoani Tabora.

Taarifa hiyo ilisema Dk. Mpango amesema serikali haitaruhusu wakulima kudhulumiwa haki yao hivyo hatua za kisheria zitachukuliwa kwa wote waliohusika.

Aidha, Makamu wa Rais aliagiza kukamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria mtuhumiwa mmoja aliyebaki wa utekaji na mauaji ya ofisa mtendaji wa kijiji cha Nyahua aliyekuwa katika majukumu yake ya kikazi.

Katika Mkutano huo, Dk. Mpango pia aliagiza Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) kukarabati miundombinu ya barabara husani barabara muhimu za kiuchumi za wilaya ya Sikonge kabla ya msimu wa mvua kuanza.

Katika hatua nyingine, Makamu wa Rais aliwasihi wananchi hao kutumia vyema siku zilizotolewa za kujiandikisha katika daftari la wapigakura kwa ajili ya kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika mwezi ujao.

Awali, Dk. Mpango aliweka jiwe la msingi la Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria kwa miji ya Sikonge, Urambo na Kaliua unaogharimu Sh. bilioni 143.2.

Makamu wa Rais alimshukuru Balozi wa India nchini, Bishwadip Dey kwa nchi yake kufadhili mradi huo mkubwa.

Alisema India na Tanzania zimekuwa na urafiki wa muda mrefu na kushirikiana katika mambo mbalimbali yakiwamo elimu, biashara, teknolojia na maji.

Dk. Mpango alisema serikali inaendelea na jitihada za kutatua changamoto za maji kwa vitendo ili kuwainua wananchi kiuchumi na taifa kwa ujumla. Alisema Sikonge kwa miaka mingi ilikabiliwa na changamoto ya majisafi na salama hivyo wananchi wanapaswa kutunza miundombinu hiyo ili huduma ya maji iweze kudumu kwa muda mrefu.

Makamu wa Rais alisisitiza kuwa mradi huo ambao umefikia asilimia 48, kutekelezwa na kukamilika kwa wakati ili wananchi waanze kunufaika.

# Waziri Lukuvi aeleza uzoefu wake vyama vingi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, William Lukuvi, ameeleza uzoefu wake katika mfumo wa vyama vingi huku akisisitiza vyama vya siasa vifanye siasa zenye madhumuni ya kudumisha amani, maelewano na maendeleo.

Aidha, ametoa wito kwa vyama hivyo kumtumia kama daraja kufikisha ushauri wao kwa mtu yeyote ndani ya serikali ili kujenga umoja na kuelewana.

Akifungua Mkutano wa Baraza la Vyama vya Siasa jana jijini hapa, Lukuvi alisema: "Niko bungeni tangu Bunge la kwanza la vyama vingi na hadi sasa kwa bahati nzuri nimebaki peke yangu. Mambo haya nayajua sana na mfumo huu naujua sana, nimeona mengi, nimeshiriki mengi tangu mwaka 1995.

"Kwa hiyo nimekuja kujitambulisha kwenu mimi ni mwenzenu tuko pamoja katika siasa. Tufanye siasa njema yenye madhumuni ya kudumisha amani, maelewano na maendeleo kwasababu vyama ni njia ya kwenda tu huko," alisema.

Aidha, alisema anafahamu kuna wakati kuna vyama vinapenda kutoa ushauri hata baada ya uchaguzi, hivyo milango yake iko wazi anawakaribisha.

"Kuna vyama vingependa kutoa ushauri kwa serikali. Unaweza kuwa na jambo la barabara, nishati ulifikishe tu kama mzalendo, sasa mlango wa kupita ni kwangu. Ninyi ambao mngependa kutoa ushauri kwa mtu yeyote ndani ya serikali, nawakaribisha mpitie kwangu, nitakuwa daraja lenu. Leteni na ushauri wa kimaendeleo kwa sababu nyie ni viongozi si tu wa vyama vya siasa lakini na maendeleo," alisema.

Lukuvi ambaye ni Mbunge wa Isimani mkoani Iringa, alisema hata kama kuna jambo wanawiwa kueleza serikali, iko tayari kuwaunganisha na huyo mwenye jambo lake unayetaka kumwambia.

"Kwa hiyo nataka kujitambulisha kwenu kama moja ya kazi niliyonayo mimi ni kuwa daraja lenu, kama kuna jambo msisubiri Baraza mmekutana, kuna mambo mnaweza kujadili hapa lakini yapo kwenye ajenda," alisema.

Alisema hata siku ambayo wana mambo yao na wanataka kualika wanasiasa wa serikalini yupo tayari kwenda.

"Hata kama ni kwa mzee wa ubwabwa (Hashim Rungwe - Mwenyekiti wa Chama cha Umma) nitakuja tu kula ubwabwa. Mimi si kiongozi wa CCM wa kuja huku kwenye baraza wanakuja viongozi wa kuchaguliwa wa chama. Lakini kwa nafasi yangu kama waziri wa siasa kwa hiyo mkiwa na siasa zenu kwenye jimbo mnasherehekea miaka 10 ya UDP mkinialika nakuja. Mnasherehekea miaka kadhaa ya fikira za kuanzishwa CHADEMA (Chama cha Demokrasia na Maendeleo) nakuja mimi," alisema.

Lukuvi alisema ndani ya serikali wana wajibu wa kushirikiana na raia yeyote na tayari ameanza ziara ya kutembelea vyama vya siasa na hadi sasa amefika kwenye vyama nane.

"Bado sijafika kwenye vyama 11, nitafika hadi kwa CCM nitakuja kuwasalimia na hii ni kulingana na ratiba zenu mkiwa na nafasi mniambie nitakuja," alisema.

Kuhusu uchaguzi wa serikali za mitaa, Lukuvi alisema ni muhimu kwa vyama vya siasa na anaamini vyama vyote 19 vitashiriki na kuhakikisha uchaguzi unakuwa mzuri.

"Rai yangu kwa viongozi wa vyama vya siasa na viongozi wengine wa dini, mila tushirikiane kukumbusha watu wetu waende kujiandikisha hii ni haki ya kila mmoja bila kujali, chama au dini, kila mmoja ana haki ya kujiandikisha na kwenda kushiriki uchaguzi, sisi kama serikali kama mlivyomsikia Rais na falsafa zake nne amesema angependa uchaguzi huu uende vizuri kwa kutunza amani iliyopo na uwe wa heshima," alisema.




Timu ya wafanyakazi wa Benki ya ICB, wakionyesha ari yao ya kutoa huduma kwa wateja, wakati wa kuadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja katika Tawi la ICB Vijana, jijini Dar es Salaam juzi. Kutoka kushoto ni maofisa waandamizi wa benki hiyo, Gloria Magwira, Sylvia Kibasa, George Rwechungura, Alex Mihayo, Kelvin Kwesigabo, Ivan Kabendera, Salesia Mpepo na Bahati Makamba. **PICHA: ICB**

## Serikali yatoa ruzuku nishati safi ya kupikia

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa ruzuku ya asilimia 50 ya bei kwa mitungi ya gesi inayosambazwa nchini na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), imebainika.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Christina Mndeme (pichani chini), alisema hayo juzi wakati wa Maonesho ya Samia Kilimo Biashara Expo 2024 yanayofanyika Gairo mkoani Morogoro.

Alisema lengo la ruzuku hiyo ni kupunguza gharama kubwa ya nishati hiyo ili kila Mtanzania amudu gharama za kuipata nishati safi ya kupikia.

"Rais Samia ni kinara wa nishati safi nchini na ndiye anayetuhamasisha kuendelea kutumia nishati safi sisi Watanzania kwa kutoa ruzuku ya bei kwa kila mtungi wa gesi hii," alisema Mndeme.

Mkuu wa Wilaya ya Gairo, Jabir Makame, aliipongeza REA kwa kuendelea kugawa mitungi ya gesi na majiko banifu kwa wananchi wa wilaya hiyo na kusisitiza elimu kuendelea kutolewa kwa matumizi sahihi.

Naye Mhandisi Deusdedit Malulu kutoka REA alitoa elimu ya nishati safi ya kupikia kuhusu umuhimu wa nishati hiyo, madhara ya matumizi ya nishati chafuzi na namna bora ya matumizi ya teknolojia ya nishati safi.

"Nimetoa elimu ya namna bora ya kutumia teknolojia ya nishati bora ya kupikia pamoja na miradi mbalimbali inayotekelezwa na REA katika miradi ya nishati safi ya kupikia," alisema.

Hadi sasa kampuni nne zimepewa zabuni na REA ya kusambaza gesi ambazo ni Orxy, Manjis, Lake na Taifa Gas. Kampuni hizo zinasambaza mitungi ya gesi kwa bei ya ruzuku.






## Wagonjwa 90 wafanyiwa upasuaji

**Na Christina Mwakangale**

TAKRIBANI wagonjwa 90 kati ya 900 waliofanyiwa matibabu ya macho, wamefanyiwa upasuaji wa magonjwa mbalimbali ikiwamo kutoa mtoto wa jicho.

Matibabu hayo yametolewa bure katika Kituo cha Afya Chalinze kwa ushirikiano wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)-Mloganzila na Taasisi ya Vision Care ya Korea Kusini.

Bingwa wa Magonjwa ya Macho kutoka MNH-Mloganzila, Dk. Audrey Mwashilemo, alisema kati ya wagonjwa 900 waliofanyiwa uchunguzi na wagonjwa zaidi ya 90 wamefanyiwa upasuaji wa magonjwa mbalimbali ya macho.

Dk. Mwashilemo aliongeza kuwa baadhi ya wagonjwa wamekutwa na changamoto mbalimbali za uoni na wamepatiwa matibabu, dawa pamoja na miwani kulingana na changamoto zinazowakabili.

"Tunawapongeza wananchi kwa kuitikia wito wa kujitokeza katika kambi hii, tumeshuhudia wananchi kutoka mikoa ya Kilimanjaro, Morogoro, Arusha, Iringa, Mbeya na Dar es Salaam wakiwa miongoni mwa wananchi waliokuja," Dk. Mwashilemo.

Baadhi ya wananchi waliojitokeza katika kambi hiyo wameishukuru MNH na Mbunge wa Chalinze, Ridhiwani Kikwete, kwa kufanikisha matibabu hayo ya bure na kwamba waendelee kuleta huduma kama hizo.

Uchunguzi na matibabu ya macho bure, umeenda sambamba na Siku ya Uoni Duniani ambayo huadhimishwa kila Jumatano ya pili ya Oktoba, kila mwaka na kauli mbiu ya mwaka huu: Yapende macho yako, mhamasishe mtoto kupenda macho yake.

# Asasi yazindua kampeni ya kutokomeza rushwa ngono

**Na Joyce Lameck**

KATIKA kupambana na rushwa ya ngono kwa wasichana na wanafunzi, taasisi isiyo ya kiserikali ya Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), imezindua kampeni ya kutoa elimu kwa jamii na madereva ili kukomesha vitendo hivyo hasa kwa wanafunzi.

Uzinduzi wa kampeni hiyo yenye kaulimbiu isemayo 'Vunja Ukimya, Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana', ulifanyika jana Bunju, Kinondoni mkoani Dar es Salaam.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Mkurungezi Mtendaji wa WAJIKI, Janeth Mawinza, alisema lengo ni kutoa elimu ya ulinzi kwa wanafunzi shuleni na kupinga vita rushwa ya ngono kwa madereva wa daladala, bajaji na bodaboda.

Mawinza alisema kampeni hiyo itajikita katika kuwashawishi wanawake kushiriki kugombea nafasi za uongozi katika Uchaguzi wa Serikari za Mitaa na hata unaohusu nafasi za juu ili kufikia lengo la 50/50.

"Tunaamini kampeni hii italeta matokeo chanya katika vitu vitatu ambavyo tumelenga katika kutoa elimu kwa madereva ambao moja kwa moja ndio wanawabeba wanafunzi na wasichana kuwatoa sehemu moja kwenda nyingine. Pia tunalenga kuwapa ushawishi wanawake kugombea uongozi na kutoa elimu ya ulinzi wa wasichana shuleni," alisema.

Mawinza alisema kampeni hiyo imeleta matokeo chanya katika Wilaya za Temeke, Ilala na Kinondoni ambapo baada ya madereva kupatiwa elimu, kumekuwa na mwitikio na mabadiliko dhidi ya ukatili wa kingono kwa wanafunzi.

Alisema wanahitaji kuwafikia wanafunzi wasiopungua 35,000 katika shule sita ndani ya Kata ya Bunju A, shule nne za msingi na mbili za sekondari na kutoa elimu kwa bodaboda wasiopungua 200 na walimu 100.

# Mwinyi asema mafanikio ya utalii yameitangaza Tanzania kimataifa

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema mafanikio makubwa yaliyopatikana katika sekta ya utalii yanayoitangaza Tanzania kimataifa na kuitambulisha duniani kuwa nchi ya kwanza Afrika na ya sita duniani inayofanya vizuri kwa utalii.

Amesema mafanikio hayo ni juhudi zinazofanywa na serikali chini ya Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuimarisha miundombinu ya utalii ikiwamo kuendelea kuiimarisha Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL),

Kwa mujibu wa Dk. Mwinyi, sababu zingine ni pamoja na kuhamasisha mashirika mengine ya ndege ya kimataifa kuanzisha safari za moja kwa moja kati ya Tanzania na nchi zenye masoko ya utalii, kujenga barabara na reli za kisasa zinazounganisha vivutio vya utalii, kujenga na kukarabati viwanja vya ndege na kuimarisha huduma zingine muhimu za utalii.

Taarifa iliyotolewa na Idara ya Mawasiliano Ikulu, Zanzibar, ilisema Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana Dar es Salaam kwenye hafla ya ufunguzi wa Onesho la Nane la Utalii la Kimataifa la Swahili.

Alisema kutokana na juhudi za Rais Samia za kukuza utalii nchini, Tanzania imeshuhudia idadi kubwa ya watalii wa kimataifa wanaotembelea sehemu mbalimbali nchini pamoja na ongezeko la mapato yatokanayo na sekta hiyo.

Dk. Mwinyi alisema pamoja na hatua hizo, serikali pia imeendelea kuweka mazingira bora ya uwekezaji ili kuvutia wawekezaji kwenye sekta ya utalii hususan eneo la huduma za malazi.

Alisema kwa mujibu wa takwimu kutoka sekta ya utalii, hadi kufikia Agosti, mwaka huu, Tanzania imepokea watalii wa kimataifa 2,026,378 ikiwa ni kiwango cha juu kabisa kuwahi kufikiwa katika historia ya Tanzania na mapato yatokanayo na sekta hiyo kufikia Dola za Marekani bilioni 3.5.

Rais Mwinyi alibainisha kuwa sekta ya utalii imeendelea kuwa nguzo muhimu katika kukuza uchumi wa Tanzania, huku ikichangia asilimia 17.2 ya pato ghafi la taifa, asilimia 25 ya mauzo ya nje na kuzalisha zaidi ya ajira milioni 1.5.

Rais Dk. Mwinyi alisisitiza kuwa mafanikio hayo yameitambulisha Tanzania kimataifa kuwa ni nchi ya sita duniani na ya kwanza Afrika kwa kuwa na ongezeko kubwa la watalii kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa Septemba, mwaka huu na Shirika la Utalii Duniani (UN Tourism).

Mafanikio mengine ya utalii kwa Tanzania, kwa mujibu wa Dk. Mwinyi, ni tuzo mbalimbali za kimataifa zilizopokewa nchini zikiashiria ubora na upekee wa vivutio vilivyomo mbali na huduma zitolewazo na sekta ya utalii.

Tuzo hizo ni Pamoja na za mwaka 2023 za "World Travel Awards (WTA)" ambao waliitambua Bodi ya Utalii Tanzania kama bodi inayoongoza Afrika, Kisiwa cha Thanda Shunghumbili, Mafia kama kisiwa binafsi kinachoongoza kwa upekee, Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro kama kivutio kinachoongoza Afrika, na Hifadhi ya Taifa Serengeti kama hifadhi ya taifa inayoongoza Afrika.

Pia alisema mtandao wa "Trip Advisor" umezitambua Hifadhi za Taifa Serengeti na Tarangire kama vivutio vya viwango vya juu Afrika mwaka jana pamoja na "Island Index" kuitaka Zanzibar kuwa kisiwa cha pili kutembelewa na watalii duniani kwa mwaka 2024.

Dk. Mwinyi alisema utalii ni sekta yenye ushindani mkubwa kimataifa, hivyo bila kuweka nguvu kubwa kwenye utangazaji, haiwezi kufikia malengo yaliyojiwekea.

Kutokana na jitihada zinazofanyika, Dk. Mwinyi alipongeza Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) kwa kazi nzuri ya kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi.



Ofisa Kilimo wa Kijiji cha Gedamar, Kata ya Galapo, wilayani Babati, mkoani Manyara, Laizer Sulle (kulia), akitoa mafunzo kwa mkulima, Fatuma Iddi kupitia shamba darasa la mazao ya mbaazi na kunde, kijijini hapo juzi, ikiwa ni utekelezaji wa mradi wa uwezeshaji wakulima kielimu na maono ya mazao na udongo (VACS), katika mikoa minne kwa ufadhili wa Taasisi ya Uendeshaji wa Mifumo ya Masoko ya Kilimo (AMDT), ikilenga kuwawezesha wakulima kutoka kilimo cha kutegemea mvua kuhamia kwenye umwagiliaji. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# Mchengerwa achekelea Rais Samia kuridhia miradi mikubwa

**Na Kulwa Mzee**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Mbunge wa Rufiji, Mohammed Mchengerwa, amesema Rais Samia Suluhu Hassan ameridhia miradi mikubwa jimboni humo ikiwamo ujenzi wa jengo la halmashauri na soko la kisasa.

Akizungumza na wananchi wa Rufiji juzi katika Viwanja vya Ujamaa, Mchengerwa alisema ujenzi wa jengo la halmashauri utagharimu Sh. bilioni 10 na wa soko Sh. bilioni 14.

"Rufiji imepanda hadhi na kuwa Halmashauri ya Mji. Tunakwenda kupata miradi mikubwa baada ya Rais Samia kuridhia kujenga jengo la halmashauri lenye ghorofa tatu na ofisi 50. Jengo hili litajengwa Ikwiriri.

"Soko la kisasa litajengwa Umwe Kati na ujenzi wake utakwenda sambamba na ujenzi wa jengo la halmashauri unaotarajia kuanza mwezi ujao," alisema.

Mchengerwa alisema soko hilo litakuwa na maduka 122, vizimba 102, eneo la kuegesha magari madogo 48, vibanda vya mama lishe zaidi ya 50, mabucha ya samaki na nyama, sehemu ya kushusha maroli 30 na maghala sita ya kutunzia mizigo.

Mchengerwa alisema wanatarajia kujenga stendi ya kisasa itakayokuwa na uwezo wa kutumiwa na mabasi makubwa 76 na madogo yakiwa ni 74, bodaboda 200, taksi 20, maduka 200, hoteli yenye vyumba 25, klabu ya burudani, maduka makubwa yatakayohudumia zaidi ya watu 70.

Kadhalika alisema kutakuwa na migahawa, benki za biashara, gereji na ujenzi utaanza baada ya kukamilika upembuzi yakinifu kwa sababu michoro imeshakamilika.

Miradi mingine aliitaja ni pamoja na kituo kipya cha afya Kata ya Umwe cha ghorofa tatu kitakachogharimu zaidi ya Sh. bilioni mbili na ukarabati wa vituo vya afya.

Mchengerwa alisema katika Kata ya Nyamwage wamepokea wawekezaji kwa ajili ya kujenga kiwanda cha sukari kitakachogharimu Sh. trilioni tatu.

"Wawekezaji wengine wamejitokeza kwa ajili ya kujenga bandari mpya Kata ya Muhoro na tayari wananchi walishafidiwa na kiasi kilichotolewa ni Sh. bilioni 2.9. Inajengwa kwa ajili ya kusafirisha ndizi na itakuwa na uwezo wa kusafirisha kontena 40 kwa siku na nyumba 400 zitajengwa," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Klabu Ligi Kuu nchini tupieni jicho michuano CECAFA U-20

**MASHINDANO** ya vijana wa umri chini ya miaka 20 ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U-20), yanafanyika hapa nchini kwa kushirikisha timu kutoka mataifa tisa ya ukanda huo.

Mashindano haya lengo lake ni kupata wawakilishi wawili watakaoiwakilisha CECAFA katika Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON U-20), yatakayofanyika baadaye mwakani.

Michuano hiyo inachezwa katika viwanja viwili ambavyo vyote viko Dar es Salaam (Azam Complex ulioko Chamazi na KMC Complex wa Mwenge).

Nchi zinazoshiriki mashindano hayo ni pamoja na wenyeji Tanzania (Ngorongoro Heroes), Kenya, Rwanda, Sudan na Djibout ambazo zimepangwa katika Kundi A huku Kundi B linaundwa na Uganda, Sudan Kusini, Burundi na Ethiopia.

Mechi za mashindano hayo bado ziko katika hatua ya makundi, nusu fainali yake itachezwa Oktoba 18, mwaka huu huku fainali yake ikitarajiwa kufanyika siku mbili baadaye na timu zitakazochuana hatua hiyo ndio zitakuwa zimekata tiketi ya kushiriki fainali za Afrika.

Kama ambavyo mashindano haya yanajieleza, yanashirikisha wachezaji chipukizi ambao wana umri chini ya miaka 20, hapa ndio sehemu nyingine sahihi ya kuangalia wachezaji wa kuwasajili kuelekea dirisha dogo na si vibaya wakati mwingine kuanza maandalizi ya msimu ujao.

Timu zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi ya Championship (zamani Ligi Daraja la Kwanza) na hata First League kwa klabu ambazo zimejipanga na zina dhamira ya kupanda daraja kuelekea msimu unaofuata, huu ndio wakati wa kutuma makocha na mawakala wenu kuangalia wachezaji wa kuwasajili kwa sababu timu itakayofanikiwa kupata mchezaji, atakuwa na umri mdogo.

Klabu itakayofanikiwa kusajili mchezaji au wachezaji kutokana na mashindano haya, basi itakuwa na uhakika kweli imenasa nyota chipukizi kwa sababu hata kama kuna 'ujanja' umetumika wa kudanganya umri, mchezaji huyo hatakuwa na umri wa zaidi ya miaka 25.

Tunazikumbusha klabu kuwa na tabia ya kutembelea mashindano yanayohusisha wachezaji vijana na kwa kufanya hivyo itawasaidia kuokoa kiasi kikubwa cha fedha za usajili pale ambapo utasubiri nyota huyo ambaye ungemsajili sana atakapokuwa ametimiza miaka 20 au zaidi.

Lakini wakati tunazikumbusha timu kwenda kuangalia vipaji, tunaamini pia licha ya sasa kuwa kwenye maandalizi ya mechi ya marudiano dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), benchi la ufundi la Timu ya Taifa (Taifa Stars), linaifuatilia kwa 'jicho kali' michuano hii kwa ajili ya kupata wachezaji watakaojiunga na timu hiyo hivi karibuni.

Tunaamini wachezaji wa Ngorongoro Heroes wanaweza kuwa nyota sahihi wa kuendelezwa kwa ajili ya kuitumikia Taifa Stars kwenye Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika zitakazofanyika hapa nyumbani mwaka 2027 (AFCON 2027), kwa sababu hadi kufika muda huo watakuwa wamepata uzoefu na wameiva tayari kupeperusha vyema bendera ya Tanzania.


Wachezaji ambao wamepita katika misingi sahihi, wanapewa nafasi ya kuipa timu matokeo chanya, na kwa sababu nyota wa sasa wa Ngorongoro Heroes, pia wamepita kwenye njia hiyo, ni wazi hadi kufikia mwaka 2027, watakuwa wako tayari kuipambania jezi ya Tanzania katika mashindano hayo makubwa hapa Afrika kutokana na uwezo ambao watakuwa wamefikia.

Njia sahihi ya kufika kwenye mafanikio ni kuwekeza kwa wachezaji vijana, timu za hapa nchini yatumieni mashindano haya yanayoandaliwa na Baraza la Soka la Afrika Mashariki na Kati (CECAFA) na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kupata wachezaji ambao watazitumikia klabu zenu na hapo baadaye kujiepusha kutumia kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya usajili.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Mashabiki waitwa uwanjani kuiongezea nguvu Taifa Stars

**BADO** kuna watu wanajiuliza kwa nini rekodi zinaonyesha Timu ya Taifa (Taifa Stars), inashinda zaidi mechi zake ugenini kuliko nyumbani?

Wapo wanaojiuliza, ni kitu gani kinaifanya pia icheze vizuri zaidi ikiwa nje ya Tanzania tofauti na wanapokuwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam?

Juzi ikiwa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo), Taifa Stars ilicheza kimkakati zaidi na mchezo huo na kama si kujifunga, ingeweza kuondoka na pointi moja muhimu ya ugenini.

Imefungwa bao 1-0, lakini ina mchezo mwingine unaotarajiwa kuchezwa Jumanne kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, katika kampeni ya kusaka tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2025), zitakazochezwa mwakani nchini Morocco.

Kwa alivyoongea Kaimu Kocha Mkuu, Hemed Suleiman 'Morocco', Stars ina uwezo wa kulipiza kisasi kama mapungufu aliyoyaona yatatatulika.

Alichokiona yeye Morocco kwa jicho lake la ufundi ni safu ya ushambuliaji kuwa butu kidogo, pamoja na utengenezwaji nafasi. Ukiangalia jinsi ilivyopambana ikiwa ugenini mbele ya Wakongomani waliokuwa jukwaani wakiishangilia timu yao, ni kweli Stars inaweza kabisa kuifunga DR Congo na kuchukua pointi tatu hapa nyumbani.

Lakini swali linakuja, rekodi inatukataa Watanzania tukicheza kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, hapa ndipo ambapo huwa tunavurugikiwa na kila mmoja anaongea lake mpira unapomalizika.

Tumeshawahi kuifunga Uganda kwao, lakini hapa tukafungwa. Tulishawahi kutoa sare DR Congo, lakini tukachapwa mabao 3-0 hapa hapa, rekodi zinaonyesha hivyo. Tatizo hasa ni nini? Ni kwa sababu wachezaji wa Stars hucheza kwa presha zaidi wanapocheza nyumbani tofauti na ugenini.

Kule wanakutana na mashabiki ambao kazi yao ni kuwashangilia na kuihamasisha timu yao tu kwa chochote kile ambacho kinatokea uwanjani.

Mashabiki wengi wa Tanzania hawashangilii, bali wanaangalia mpira, na kupiga mayowe ya kushangilia kwenye matukio fulani fulani machache kama goli likikoswa, kanzu, chenga, tobo, au mbwembwe tu za baadhi ya wachezaji.

Ninachoona bado mashabiki wa Tanzania hawajaanza kuwa sehemu ya kuwatafutia wachezaji wao ushindi kama mashabiki wa nchi nyingine.

Wachezaji wanacheza kwa woga ili wasikosee kwa sababu mashabiki wamekuwa na lawama mno kuliko kuiunga mkono timu hiyo. Cha ajabu mashabiki hawa hawa zikicheza timu zao pendwa za Simba au Yanga, wanafanya kile kilichowapeleka uwanjani, nacho kuwa sehemu ya kuwatoa mchezoni wapinzani na kuchangia ushindi kwa timu yao.

Linapokuwa suala ya taifa, wanawaacha wachezaji wafanye wenyewe, wao wapo uwanjani wakisubiri ushindi ili washangilie.

Ifike wakati sasa mashabiki wa Tanzania wasiende uwanjani kuangalia nani anakosea na ni wa timu gani ili amkosoe, badala yake kuwa sehemu ya kuchangia ushindi. Kushangilia mwanzo hadi mwisho, kutawapa moyo wachezaji wanapokosea, badala ya kuanza kulaumu, kuwatoa mchezoni wapinzani wanapokuwa na mpira, kuwahimiza kufanya mashambulizi badala ya kuchekelea chenga na vingine visivyo vya msingi.

Wakifanya hivi Jumanne, kuna uhakika ka wa kuifunga DR Congo na kujiweka katika mazingira mazuri ya safari ya kuelekea AFCON hapo mwakani.

Namna Kundi H lilivyo, endapo Stars, ikichukua pointi tatu kutoka kwa Wakongomani keshokutwa basi sidhani kama kuna timu ya kuizuia kwenye mbio hizo ambazo pia zinawaniwa na Ethiopia yenye pointi moja huku Guinea ambayo haina pointi hata moja ikiburuza mkia.

> **Ifike wakati sasa mashabiki wa Tanzania wasiende uwanjani kuangalia nani anakosea na ni wa timu gani ili amkosoe, badala yake kuwa sehemu ya kuchangia ushindi.**

HABARI KITAIFA

# Ukosefu wanawake kwenye uongozi chanzo cha kuporomoka kwa maadili

**Na Thobias Mwanakatwe,**

SINGIDA

SPIKA wa Bunge mstaafu, Anne Makinda, amesema kukosekana kwa maadili katika jamii kunatokana na wanawake wengi kutokuwapo katika nafasi za uongozi.

Amesema kutokana na hali hiyo katika uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika Novemba 27, mwaka huu, na uchaguzi mkuu utakaofanyika mwakani, wanawake wachukue fomu kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

Makinda alisema hayo juzi wakati wa Tamasha la Wanawake na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa lililofanyika kwenye viwanja vya Bombadia, mjini hapa na kuwashirikisha wanawake kutoka wilaya zote za mkoa wa Singida.

"Mambo ya kukosa maadili ni kwa sababu nyie wanawake hampo katika uongozi. Kwa hiyo nawaomba uchaguzi wa serikaii za mitaa na uchaguzi mkuu gombeeni," alisema.

Makinda alisema wanawake wengi wakiwa viongozi, hata amani iliyopo nchini itaongezeka maradufu na kutajenga misingi ya upendo na amani.

Alisema wanawake watakapogombea uongozi wakati wa kujaza fomu wasiwe pekee yao watafute watu ili kuepuka kufanya makosa ambayo yatasababisha wawekewe pingamizi.

Makinda ambaye ni Kamisaa wa Sensa, alisema suala la kushindwa wanawake waliondoe katika vichwa vyao watakapogombea uongozi kwenye chaguzi hizo.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, alisema uwakilishi wa wanawake katika nafasi mbalimbali za uongozi katika mkoa wa Singida ni mdogo hasa katika vitongoji 2,000 vilivyoko, wanawake kwenye uongozi ni asilimia nne tu.

Alisema katika vijiji 441 vya mkoa wa Singida ni wanawake watano tu ndio walipata nafasi ya uongozi kuwa wenyeviti ambao ni sawa na asilimia moja wakati katika kata 136, ni kata nne tu ndizo walioch- aguliwa kuwa madiwani.

"Katika Manispaa ya Singida kuna mitaa 53 lakini wanawake waliothubutu kuchukua fomu na kushinda ni watatu tu wakati katika nafasi ya ujumbe kati ya nafasi 11,000 za wajumbe wa serikali za mitaa wanawake 3,125 ndio wajumbe wa serikali za mitaa," alisema.

Dendego alisema kutokana na uwakilishi mdogo wa wanawake katika uongozi, serikali ya mkoa wa Singida imeona haiwezi kunyamazia suala hilo, hivyo imeamua kuandaa kongamano ili kuwapa uelewa na ujasiri wanawake kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa.



Mwenyekiti wa Kamati ya Maonesho ya Siku ya Wakulima wa Miwa Bonde la Kilombero, ambaye ni Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa wadau wa Kilombero Sugar, Victor Byemelwa (wa pili kushoto), akimsikiliza Mbunge wa Jimbo la Kilombero, Abubakari Assenga, alipowasili katika mdahalo uliwakutanisha wadau kutoka sekta mbalimbali za sukari, wilayani Kilombero, mkoani Morogoro, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbaroni tuhuma mauaji dereva bodaboda

**Na Ashton Balaigwa.**

JESHI la Polisi mkoani Morogoro linawashikilia watu wanne kwa tuhuma za mauaji ya dereva wa bodaboda, Shaban Mwawile (18), mkazi wa Lipangalala Wilaya ya Kilombero baada ya kumpora pikipiki yake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Alex Mkama, alisema tukio hilo lilitokea Septemba 8, mwaka huu, wilayani Kilombero.

Alisema awali zilitolewa taarifa na ndugu kuwa kijana huyo amepotea ndipo Jeshi la Polisi lilipoanza ufuatiliaji na ilipofika Septemba 29, watuhumiwa wote wanne walikamatwa kuhusiana na mauaji hayo.

Kamanda Mkama aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Athuman Mpango (38) fundi ujenzi mkazi wa Ifakara, Denis Swai (34) mkulima mkazi wa Mofu, Mussa Bushiri (28) mkulima mkazi wa Upogoroni na Alhaji Likwaya (32) mkulima na mkazi wa Michenga.

Alisema watuhumiwa hao baada ya kufanyiwa mahojiano ya kina, walikiri kuhusika na mauaji ya kijana huyo, kisha kuwaongoza askari mpaka kwenye kambi ya Senga iliyoko katika pori la akiba la Kilombero, Kata ya Minepa Wilaya ya Ulanga walipoutelekeza mwili ambao ulikutwa umeharibika.

Kamanda Mkama alisema upelelezi wa tukio hilo unaendelea na watuhumiwa watafikishwa mahakamani baada ya kukamilika.

Katika tukio lingine, Polisi Morogoro wanamshikilia Said Mada (28) mkazi wa kijiji cha Malu, wilayani Kilosa na wenzake watatu kwa tuhuma za kuhusika na unyang'anyi wa kutumia silaha.

Mkama alisema tukio hilo lilitokea usiku Agosti 7, mwaka huu, katika kitongoji cha Makale Magole, Tarafa ya Turiani, wilayani Mvomero, alisema watuhumiwa walimvamia Kulwa Magale (49) mfanyabiashara wa Kokoa akiwa nyumbani kwake.

Alisema watuhumiwa hao walitumia silaha inayosadikika kuwa gobole na panga kisha kumnyang'anya Sh. milioni 20.

Watuhumiwa hao, alisema pia walikamatwa wakiwa na silaha aina ya shotgun na watafikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.

## Vijana wapewa mchongo mafunzo huduma za ndege

**Na Joseph Mwendapole**

MKURUGENZI Mtendaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL), Ladislaus Matindi, amewataka vijana kuchangamkia mafunzo ya wahudumu wa ndani ya ndege (cabin crew) kwani kuna ajira za kutosha kwenye mashirika ya ndani na nje.

Aliyasema hayo hivi karibuni wakati wa mahafali ya wanafunzi 56 waliohitimu kozi ya wahudumu ndani ya ndege katika Chuo cha Kampuni ya Ndege Tanzania (ATTC) na kutunukiwa vyeti.

Idadi hiyo ya wanafunzi imetokana na mchujo mkali uliofanyika ambapo mchujo wa kwanza walikuwa wanafunzi 180, mchujo wa pili wakabaki 120 na waliofuzu ni 56 pekee.

Akizungumza kwenye mahafali hayo, Matindi alisema wanafunzi hao pekee ndio waliofaulu bila kuacha shaka.

Alisema jukumu kubwa la wafanyakazi wa ndani ya ndege ni kusimamia usalama wa abiria na mali zao pamoja na chombo wanachokihudumia na kwamba katika kutekeleza majukumu hayo, huduma bora kwa wateja ni kipaumbele.

"Wanafunzi wengi wanaomaliza kwenye chuo hiki wamekuwa wakipata ajira mapema zaidi katika mashirika ya ndani na nje ya nchi kutokana na kukidhi vigezo vya soko la ajira la kimataifa na wengine wameajiriwa kwenye mashirika makubwa ya ndege ya kimataifa," alisema.

Kutokana na ukuaji wa sekta ya anga duniani, alisema kumekuwa na ongezeko kubwa la maombi ya kujiunga na kozi hiyo na kwamba ongezeko la ndege za ATCL za kisasa, wakufunzi wabobezi na vifaa vya mazoezi kumechangia ongezeko la watu wengi kuwasilisha maombi ya kujiunga na kozi hii kupitia ATTC ili kutimiza ndoto zao.

Matindi alisema ATCL ina mpango wa kufungua matawi mengine nje ya Dar es Salaam ili kufikia mahitaji makubwa ya wadau wake.

Mkuu wa Chuo hicho, Elly Ndekile, alisema tangu chuo hicho kianze kutoa mafunzo ya aina hiyo, tayari wameshatoa wahitimu wataalamu zaidi ya 700 kutoka chuoni hapo.

Hafla hiyo ilifanyika mwishoni mwa wiki iliyopita katika chuo hicho kilichoko katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), Terminal One, Dar es Salaam.

# Wadau waridhishwa na huduma za bandari

**Na Joseph Mwendapole**

WADAU mbalimbali na watumiaji wa huduma za bandari wameridhishwa na ubora wa huduma sambamba na utendaji kazi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) wakisema mamlaka imefanikiwa kukidhi matarajio ya wateja wake pamoja kuyafikia malengo iliyojiwekea.

Wakizungumza katika kilele cha wiki ya huduma kwa wateja jijini Dar es Salaam jana, mmoja wa wadau hao, Hassini Norana, aliipongeza serikali kwa kuridhia uwekezaji katika Bandari ya Dar e Salaam.

"Huduma za bandari zimeimarika sana sambamba na kuwapo kwa ufanisi mkubwa. Ninaipongeza TPA kwa kufanya maboresho makubwa," alisema Norana na kuitaka TPA kuendelea kuzitangaza bandari zake.

Naye Mdau wa kutoka Bandari Kavu, Deogratius Chacha, alipongeza ufanisi na utendaji uliopo kwenye Bandari ya Dar es Salaam na kuipongeza menejimenti ya mamlaka hiyo kwa maboresho makubwa.

"Uwekezaji mkubwa uliofanywa kwenye Bandari ya Dar es Salaam na zile zilizoko kwenye maziwa ni ushahidi tosha kuwa TPA imejipanga vizuri kuleta mageuzi makubwa kwenye bandari zake," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Masoko na Uhusiano wa TPA, Dk. George Fasha, aliyemwakilisha Mkurugenzi Mkuu, Plasduce Mbossa, kwenye hafla hiyo, aliwashukuru wadau na watumiaji wote wa bandari kwa kuendelea kuiamini na kutumia bandari zilizoko nchini.

"Nikiri kuwa TPA tunauthamini sana mchango wenu kwani ni moja ya chachu inayofanikisha maendeleo ya mamlaka na taifa kwa ujumla wake," alisema na kuongeza kuwa TPA imefanya maboresho makubwa na ya kisasa katika bandari zote.

Dk. Fasha amesema TPA kwa kipindi cha mwaka 2023/24 imehudumia meli 4,487 na zilikuwa na shehena milioni 27.6. katika shehena hiyo, makasha yalikuwa milioni 11 na kuhudumiwa katika magati yote mawili sambamba na bandari za Tanga na Mtwara.

"Pamoja hayo mamlaka bado imeelekeza juhudi zake katika kuboresha miundombinu ya bandari zote ili kukidhi mahitaji ya soko linalobadilika na kukua kwa kasi huku likiwa na ushindani mkubwa toka bandari shindani," alisema.

Dk. Fasha alisema bado uboreshaji wa huduma mbalimbali unaendelea ikiwamo kujenga gati la mita 450 kwenye Bandari ya Tanga kwa jumla ya gharama ya bilioni 429.1 na kuondoa tatizo la 'double handling' na pia kupunguza msongamano katika Bandari ya Dar es Salaam.

Dk. Fasha pia alibainisha kwa wateja kuwa TPA ina mipango na mikakati kabambe ya kuanza ujenzi wa miundombinu ya kupokea na kuhifadhi mafuta ili kupunguza muda wa kuhudumia meli nangani kutoka siku nane hadi 10 mpaka kufika siku tatu kwa meli zenye ujazo wa 150,000 DWT na kupunguza gharama za ucheleweshaji wa meli.

"Tunatarajia kuanza ujenzi gati namba 12 hadi 15 katika Bandari ya Dar es Salaam kukabiliana na uhaba na magati ili kwenda sambamba na ongezeko la meli na shehena. Magati hayo yalikuwa na uwezo wa kuhudumia makasha 1,350,000 kwa mwaka," aliongeza.

## Zanzibar yapunguza uagizaji mboga, matunda

**Na Ashton Balaigwa,** ZANZIBAR

UZALISHAJI wa mazao ya mboga na matunda Zanzibar umeongezeka, hivyo kupunguza hali ya utegemezi wa kuagiza mazao hayo kutoka asilimia 80 hadi asilimia 20 kwa wafanyabiashara Tanzania Bara.

Mapinduzi hayo ya uzalishaji wa mboga na matunda yametokana na wakulima Zanzibar kupokea teknolojia za kilimo bora kupitia mradi wa kukuza kilimo Zanzibar uliokuwa unatekelezwa na Taasisi ya Kilimo cha Mboga na Matunda (TAHA) na Agri Connect.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kuhusu ongezeko la uzalishaji huo kupitia mradi wa Kukuza Kilimo Zanzibar (KUZA) baadhi ya wakulima katika vijiji vya mkoa wa Kusini Unguja walisema umeleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi katika sekta ya kilimo visiwani hapa.

Mmoja wa wakulima hao, Kashinje Mlekwa, kutoka kijiji cha Umbuji Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja, alisema uzalishaji huo umeongezeka baada ya kupatiwa mafunzo na TAHA kuhusu mboga na matunda, hivyo kuondokana na kilimo cha awali ambacho uzalishaji wake ulikuwa duni.

"Kwenye kilimo cha awali tulikuwa kama tunasukuma tu kutokana na wengi hatukuwa na elimu, hivyo uzalishaji wake ulikuwa mdogo sana. Lakini baada ya kupewa mafunzo ya kilimo bora na TAHA kila wiki tunatembelewa na maofisa ugani kwa ajili ya utaalamu zaidi na sasa tumeongeza uzalishaji," alisema.

Mlekwa alisema baada ya elimu hiyo, ameongeza uzalishaji kwenye kilimo cha mboga na matunda, hivyo kumwezesha kuinuka kiuchumi, kujenga nyumba ya kisasa na kusomesha watoto kwenye shule mbalimbali.

Naye Suleiman Nassor Suleiman, alishukuru mradi wa KUZA kwa kuwaunganisha na TAHA kwa kuongeza uzalishaji wa mboga na matunda ambao umesaidia sasa kuwa na soko kubwa la mazao hayo visiwani Zanzibar.



Kaimu Mkurugenzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Abed Gallus Abed (kushoto), akiwa na Mkurugenzi wa Masoko na Uhusiano TPA, Dk. George Fasha, wakikata keki katika kilele cha Wiki ya Huduma kwa Wateja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Wafanyabiashara wapongeza mazingira rafiki ya uwekezaji

**Na Elizabeth Zaya**

JUKWAA la Wafanyabiashara na Huduma (JBH) limempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji na wafanyabiashara nchini.

Pongezi hizo zimetolewa na Katibu Mtendaji wa Jukwaa hilo, Fredy Leopold, wakati wa uzinduzi JBH uliofanyika juzi Dar es Salaam.

Leopold alisema wafanyabiashara nchini wanatambua kazi kubwa inayofanywa na Rais Samia hususani katika kutatua kero zote ambazo zimekuwa zikilalamikiwa na wafanyabiashara hao kwa muda mrefu ikiwamo urasimu na utitiri wa kodi.

"Tunatoa shukrani zetu kwa Rais Samia na serikali kwa kazi kubwa wanayofanya, lakini kwa kutambua umuhimu wa sekta hii na kuimarisha mazingira ya biashara kuendelea kuimarisha miundombinu na kuinua wafanyabiashara nchini kupitia sera rafiki ambazo serikali imeweka kwa sasa.

"Tumeshuhudia ikiendelea kuchukua hatua madhubuti katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji kupitia uboreshaji miundombinu, kuweka sera za kifedha na kupunguza urasimu katika sekta hii.

"Tumeshuhudia pia ikianza mchakato wa kuunganisha mifumo, kukamilisha miradi ya reli ya kisasa, upanuzi wa bandari na uwekezaji katika sekta ya nishati, ni kielelezo tosha cha dhamira ya serikali katika kusaidia wafanyabiashara nchini," alisema.

Alisema wafanyabiashara hawawezi kusahau kazi kubwa iliyofanyika, hasa katika kuweka na kujenga misingi thabiti kwao.



# Vikwazo uhifadhi wa mazingira vyaanikwa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WADAU wa mazingira wametaja changamoto mbili zinazokabili utunzaji wa miti nchini ikiwamo suala la uchomaji wa moto miti wakati wa kiangazi.

Changamoto nyingine ni mifugo kuharibu miti inayopandwa ambayo hujitokeza kwa kiasi kikubwa mijini.

Meneja wa Kanda ya Kati Rasilimali Misitu wa Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), Husna Msagati, aliyasema hayo jana wakati wa upandaji wa miti katika Shule ya Msingi ya Kiwanja cha Ndege jijini Dodoma.

Upandaji wa miti huo ulifadhiliwa na Taasisi ya Fedha ya Enterprise Finance Limited (EPL), kama sehemu ya Mpango wa Kurejesha kwa Jamii (CSR) na kusema TFS inategemea miti iliyopandwa katika shule hiyo kutunzwa.

Alisema wanajua adui wa miti ni kukosa maji na moto, changamoto ambayo imekuwa ikijitokeza katika kipindi cha kiangazi kwenye maeneo mengi nchini.

"Kwa elimu tuliyoitoa katika shule hii ni matumaini yangu kuwa miti hii itatunzwa kwa kunyeshewa maji, kupaliliwa na kuwekewa mazingira ya kuhakikisha inakuwa mazuri," alisema.

Naye Ofisa Mazingira Mkuu kutoka Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Innocent Makomba, alisema 'Kampeni ya Soma na Mti' inaleta tija katika suala la utunzaji wa mazingira.

Alisema hilo linatokana na kuwa mwanafunzi anajengewa uwezo wa kutunza mazingira kuanzia akiwa bado mdogo hadi anapokuwa mkubwa na kuiona faida ya miti kadri anavyokua.

"Lakini katika kutunza kumekuwa na mambo yanayorudisha nyuma kwenye utunzaji wa miti hasa hapa mjini kwa mfano ufugaji holela wa mifugo. Hapa tunapopanda miti kama tutakuwa tunaachia mifugo yetu holela hatuwezi kuona hayo matunda ya hiyo miti," alisema.

# Chanzo watoto kutotimiza ndoto zao chabainishwa

**Na Paul Mabeja,** BAHI

VITENDO vya ukatili wa kijinsia vikiwamo ndoa za utotoni na ubakaji, vimetajwa kuwa chanzo cha watoto wengi wa kike kushindwa kufikia ndoto zao walizojiwekea.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Msichana Inatiative, Rebecca Gyumi, alibainisha hayo juzi kwenye tamasha la Msichana Amani lililofanyika katika kijiji cha Lukali, wilayani hapa ikiwa sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike Duniani.

Gyumi alisema kwa mujibu wa takwimu za Jeshi la Polisi kuhusu ukatili kwa mwaka 2023, kulikuwa na matukio ya ukatili kwa watoto takribani 15,000 kulinganisha na mwaka 2022 ambao yalikuwa 12,000.

Alisema takwimu zinaonesha kuwa katika matukio 10 ukatili, manane yametokea kwa watoto wa kike.

Gyumi alisema vitendo vya kikatili kwa watoto wa kike nchini vimekua sababu kubwa ya mtoto wa kike kushindwa kufikia ndoto zake ikiwamo kuwa viongozi katika ngazi mbalimbali za uamuzi.

"Kumekuwapo na matukio mengi ya kikatili kwa watoto hali ambayo imechangia kwa kiasi kikubwa watoto wengi wa kike kushindwa kufikia ndoto zao ikiwamo kuwa viongozi katika ngazi za uamuzi," alisema.

Alisema kama taifa linataka kuwa na viongozi wa baadaye, lazima kila mmoja aweke ulinzi kwa mtoto hasa wa kike.

"Kila mtu ana wajibu wa kuweka ulinzi kwa watoto ili mtoto wa kike afikie ndoto zake kwani kumekuwapo na matukio mengi ya ukatili yakiwamo ubakaji, ulawiti na mimba za utotoni zinazoharibu ndoto za watoto wengi wa kike," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Ofisa Tarafa ya Mndemu, Isaya Matata, aliitaka jamii kumwandaa mtoto mapema kwa kumpa nafasi ya kupata elimu na kumjenga katika misingi ya kujiamini kukabiliana na changamoto mbalimbali.

"Jamii inapaswa kubadilika kuwalinda na kuwajali watoto wa kike ili kutimiza ndoto zao kwa kuwapeleka mapema shuleni na mzazi ukiona mtoto ana kipaji ni vyema kumwendeleza kwa kumpa elimu na ulinzi wa kutosha," alisema.

Veronika Thomas, mwanafunzi wa Shule ya Msingi Lamaiti, wilayani hapa, alitoa wito kwa wazazi na walezi kuwalinda watoto wao ili kutimiza ndoto zao.



Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, mkoani Singida, Thomas Apson, akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Mpando juzi, wakati wa mkutano wa hadhara wa kuwahamasisha kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajia kufanyika Novemba 27, mwaka huu. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Serikali yahimiza ulinzi wa vyanzo vya maji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imewataka wadau wa sekta ya maji, kuweka mikakati ya kukabiliana na uvamizi wa vyanzo vya maji, uharibifu na uchafuzi wa mazingira ili kusaidia kulinda rasilimali hizo kwa miaka 25 ijayo.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Mwajuma Waziri, alisema juzi wakati akifungua kongamano la kupokea maoni ya kuboresha Dira ya Taifa kutoka kwa wadau mbalimbali wa sekta ya maji nchini.

Alisema azma ya serikali ni kuhakikisha maji safi na salama yanapatikana kwa asilimia kubwa vijijini na mijini, hivyo maoni watakayotoa yazingatie katika misingi hiyo ili kusukuma gurudumu la maendeleo katika sekta hiyo.

Alisema serikali inathamini mchango mkubwa unaotolewa na wadau wa maendeleo wa mashirika ya ndani na nje ya nchi hivyo kila mmoja ashiriki kutoa maoni yake ambayo yatafanyiwa kazi.

"Serikali inatambua mchango mkubwa, unaotolewa na wadau wa maendeleo hivyo kila mdau anapaswa kutoa maoni ili kufikia malengo yaliyokusudiwa kwenye uboreshaji wa sekta hiyo," alisema.

Alisema malengo ya Dira ya Maendeleo ni kuwafikishia maji safi na salama wananchi wa vijijini na mijini, hivyo kutokana na uzoefu walio nao wadau hao, anaamini watatoa maoni yenye mlengo chanya wa kuboresha sekta ya maji.

Katibu Mkuu hyo alisema serikali itaendelea kushirikiana na wadau katika kuendeleza sekta ya maji na kuhakikisha maoni yao katika dira ya maendeleo ya 2050 yatazingatiwa na kuyawasilisha Tume ya Mipango inayoratibu kazi hiyo.

"Mafanikio ya sekta maji yanatokana na mchango mkubwa unaotolewa na wadau, washirika wa maendeleo na taasisi za fedha nje na ndani ya nchi. Naamini kila mmoja atashiriki kutoa maoni," alisema.

Mkurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara ya Maji, Prosper Buchafwe, alisema mipango yao ya Dira ya Maendeleo 2050 ni kuhakikisha miundombinu ya maji inaboreshwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Alisema wamejipanga kuhakikisha wanachimba mabwawa ya kusaidia kupunguza adha ya uzagaaji wa maji katika maeneo mbalimbali hususani kipindi cha mvua. Pia alisema wataendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kufikia malengo yaliyowekwa na serikali kwenye sekta ya maji.

Naye Mkurugenzi wa Uandaaji Miradi, Uratibu na Usimamizi wa Mazingira, Dorisia Mulashani, alisema maoni ya wadau wa Wizara ya Maji yatasaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha maisha ya Watanzania kwa ujumla.





# Hemed asisitiza wafanyabiashara Pemba kutumia Bandari ya Mkoani

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amewataka wafanyabiashara kisiwani Pemba kuona umuhimu wa kuitumia Bandari ya Mkoani kwa ajili ya kusafirishia mizigo wanayoingiza kwa ajili ya biashara kisiwani hapa.

Hemed aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wafanyabiashara wa Pemba ofisini kwake, Tibirinzi Wilaya ya Chakechake, Pemba.

Alisema azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) chini ya Rais Dk. Hussein Mwinyi ni kuifungua Pemba kiuchumi na kuweka usawa kwa wafanyabiashara na upatikanaji wa huduma katika sekta zote zikiwamo za bandari.

Hemed alisema hali hiyo itazidisha umoja na mshikamano kwa wananchi na wafanyabiashara wa pande zote za Unguja na Pemba.

Kwa mujibu wa Hemed, serikali itaendelea kusimamia maslahi ya wafanyabiashara wa Zanzibar na usalama wa mizigo yao na iwapo kutakuwa na changamoto ya aina yoyote, serikali kupitia vyombo husika itazitatua kwa haraka zaidi.

Aidha, Hemed aliagiza Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) Ofisi ya Pemba kuwapa mafunzo wafanyakazi ili kuimarisha utendaji wao wa kazi kwa wafanyabiashara walioko kisiwani hapa pamoja na kutoa elimu kwa wafanyabiashara kwa kuhamasisha kulipa kodi kwa hiari.

Alisema elimu hiyo itasaidia kuendelea kuziamini na kuzipa ushirikiano taasisi zinazosimamia kodi nchini.

Wafanyabiashara kisiwani Pemba waliishukuru serikali kwa mambo mazuri ya maendeleo yanayoendelea hasa kwa azma ya kuifungua Pemba kiuchumi ikiwamo kuifungua Bandari ya Mkoani.

Abdallah Said, mmoja wa wafanyabiashara hao, alisema changamoto kubwa inayowakabili ni kodi kubwa wanayotozwa na mamlaka husika, hivyo kuiomba serikali kuliangalia kwa umakini suala hilo ambalo limekuwa likipunguza ari na mwamko wa ufanyaji wa biashara kisiwani Pemba.

Naye Rashid Manyimbo, alisema endapo serikali itaandaa utaratibu na mazingira mazuri kwa wafanyabiashara wa Pemba, wana imani kuwa malengo ya viongozi wakuu ya kuifungua Pemba kiuchumi yatafanikiwa.

Pia alisema hali hiyo itawezesha kulipa kuwa wanalipa kodi kwa wakati kwa kuwa taifa lolote duniani linategemea kodi ili kupata maendeleo.



Waziri wa Maji, Jumaa Aweso (katikati) pamoja na Mkurugenzi wa Usambazaji Maji wa Wizara ya Maji, Joyce Msiru (wa tatu kushoto), wakionyesha ripoti ya Maji inayolenga kukabiliana na changamoto za usalama wa maji, baada ya kukabidhiwa jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Breweries Limited Michelle Kilpin (wa tatu kulia), Mwenyekiti wa Bodi ya TBL, Leonard Msusa (kushoto) na Mkurugenzi wa WWF nchini, Dk. Amani Ngusaru. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mfumuko wa bei za bidhaa washuka

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KASI ya kiwango cha mfumuko wa bei wa mwaka ulioishia Septemba 2024, imepungua kufikia asilimia 4.76 kutoka asilimia 5.12 iliyorekodiwa Agosti, mwaka huu.

Mtakwimu Kitengo cha Takwimu za Bei, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS), Hassan Jamal Hassan, alisema alipokuwa akiwasilisha taarifa hiyo kwa waandishi wa habari, Mazizini jana.

Alisema hiyo ilichangiwa zaidi na bei za bidhaa za vyakula na vinywaji visivyo na kileo kupungua kwa asilimia 7.15 Septemba, 2024 ikilinganishwa na asilimia 8.69 iliyorekodiwa katika Agosti.

Hassan alisema kwa ujumla faharisi za bei ziliongezeka na kufikia 113.33 kwa Septemba 2024 ikilinganishwa na 108.18 ambayo iliripotiwa katika mwezi Septemba, mwaka jana.

Alizitaja bidhaa zilizosababisha kupungua kwa mfumuko wa bei na asilimia kwenye mabano kuwa ni mchele wa Mapembe (3.5), mchele wa Mbeya (9.3), mchele wa Basmati (2.3), unga wa ngano (5.6), unga wa sembe (8.3), ndizi mtwike (37.3), sukari nyeupe (2.7) na sukari nyekundu (8.7).

Kwa mujibu wa mtakwimu huyo, mfumuko wa bei wa bidhaa za chakula wa mwaka ulioishia Septemba 2024, ulipungua na kufikia asilimia 7.29 ikilinganishwa na asilimia 8.88 iliyorekodiwa katika Agosti 2024.

Aidha, alisema mfumuko wa bei za bidhaa zisizo za chakula kwa mwaka uliongezeka na kufikia asilimia 2.83 kwa mwezi Septemba ikilinganishwa na asilimia 2.32 kwa mwezi Agosti.

Alisema mfumuko wa bei wa Septemba 2024, uliongezeka na kufikia asilimia 0.61 ikilinganishwa na asilimia 0.30 iliyorekodiwa katika mwezi Agosti 2024.

Mfumuko wa bei wa bidhaa za chakula na vinywaji visivyo na kileo kwa mwezi Septemba, ulipungua na kufikia asilimia 0.68 ikilinganishwa na asilimia 0.89 iliyorekodiwa Agosti 2024.

Alizitaja bidhaa zilizosababisha kuongezeka kwa mfumuko wa bei na asilimia kwenye mabano kuwa ni mchele wa basmati (0.7) mafuta ya kupikia ya OKI (4.6) na mafuta ya petroli asilimia 3.3.

Mchumi Mhadhiri Mwandamizi wa Shule ya Biashara ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Dk. Estella Ngoma Hassan, alisema kupungua kwa kasi ya mfumuko wa bei ni hatua nzuri ya kiuchumi na malengo yaliyokuwapo ya kubakia kwenye tarakimu moja.

"Ni ahueni kwa wananchi na hii inatokana na kuwapo kwa bidhaa za kutosha kwenye masoko," alisema Dk. Ngoma.

Mfumuko wa bei ni kipimo kinachotumika kupima mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma mbalimbali zinazokusanywa katika masoko ya miji ya Zanzibar.

## Maktaba Z'bar yazawadiwa vitabu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KITUO cha Utamaduni cha Russia nchini Tanzania kimekabidhi vitabu 100 kwa Bodi ya Huduma za Maktaba Zanzibar, ikiwa ni msaada kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ).

Hafla ya makabidhiano ya vitabu hivyo vyenye jina la Malkia wa Tufufu, ilifanyika katika Maktaba Kuu Zanzibar, Maisara, Mjini Unguja.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mwakilishi Mkazi wa Kituo hicho, Rifat Pateev, alisema utoaji wa vitabu hivyo ni mwendelezo wao wa kuisaidia Zanzibar ili kutumika katika maktaba zote za Zanzibar.

Kwa mujibu wa mwakilishi huyo, ushirikiano uliopo baina yao na watendaji wa huduma za maktaba ni wa kupongezwa na unapaswa kuendelezwa.


Alisema kituo chao kitaendelea kutoa ushirikiano na serikali katika kuimarisha maendeleo ya elimu.

Naye Mkurugenzi wa Bodi ya Maktaba Zanzibar, Ulfat Abdulaziz, alisema kituo hicho kina utamaduni wa kuwapatia vitabu mbalimbali ambavyo hutumika katika maktaba zao.

Alisema vitabu ambavyo wamepatiwa watahakikisha wanavitumia kwa malengo yaliyokusudiwa ikiwamo kuvieneza katika maktaba zote zilizoko Zanzibar.

"Leo mmetuletea vitabu lakini hii si mara ya kwanza tumeshapokea vitabu vingi sana kutoka kwenu. Lakini kupitia ninyi tumeshafanya maonesho ya vyuo vikuu vilivyoko Russia na Wazanzibari wamepata fursa mbalimbali za kujua fursa za masomo zinazopatikana katika vyuo hivyo," alisema.

Ulfat alisema anaamini ushirikiano huo utaendelea na watazidi kushirikiana kwa maslahi ya nchi zao na wao pamoja na kuvipokea lakini pia watavisambaza kwa wengine ili waweze kujifunza zaidi.



ZUCHU
UKURASA 12

JUMAMOSI OKTOBA 12, 2024



# Diamond tena tuzo MTV EMA

Nyota wa muziki wa Bongo Fleva na Afrika Mashariki, Diamond Platnumz, ameteuliwa kuwania tuzo zinazotambulika kimataifa, MTV Europe Music Awards (EMA) 2024.

Mwimbaji huyo amechaguliwa katika kipengele cha "Best African Act", akichuana vikali na wasanii wengine wenye majina makubwa barani Afrika, akiwamo Asake na Ayra Starr kutoka Nigeria, Tyla, Titom & Yuppe, na DBN Gogo kutoka Afrika Kusini.

Hii si mara ya kwanza kwa Diamond kuwania tuzo hizi zinazoenzi wasanii bora duniani. Mwaka 2023, aliibuka mshindi katika kipengele hicho hicho, akiwa msanii pekee kutoka Afrika Mashariki aliyeteuliwa. Ushindi huo ulikuwa wa kihistoria kwake na kwa Tanzania kwa ujumla, ukimshuhudia akipambana na majina makubwa kama Burna Boy na Asake kutoka Nigeria.

Diamond ana historia nzuri linapokuja suala la tuzo za MTV EMA. Mwaka 2015, aliweka rekodi ya kuwa msanii wa kwanza Afrika kushinda tuzo tatu za EMA ndani ya usiku mmoja. Alishinda tuzo ya "Best African Act", "Best Worldwide Act (Africa/India)", na "Best African Act" tena mwaka jana, 2023.

BASI SAWA

## Rosa Ree kumbe kiungo mkabaji



RAPA wa kike nchini, Rosa Ree, amesema kama asingekuwa msanii, basi angekuwa mcheza mpira wa miguu na angecheza moja ya timu za Ligi Kuu Tanzania Bara kwa wanawake.

Msanii huyo ambaye ametoa ngoma kali na za kuvutia kama 'Mama Omollo', 'Blessed' na nyingine nyingi alisema zamani alikuwa anacheza soka kabla ya kuanza masuala ya muziki.

"Mimi kabla ya kuwa msanii nilikuwa mcheza soka mzuri tu na leo hii kama si muziki ningekuwa nacheza mpira kwenye moja ya timu ya Ligi Kuu ya Wanawake nchini," alisema.

Alisema alikuwa akicheza nafasi ya namba sita, kiungo mkabaji, maarufu kama mkata umeme.

"Ndiyo maana mwanangu anapenda sana kucheza mpira, nadhani anaweza kuwa mwanasoka mzuri tu hapo baadaye," alisema.

## Zuchu, Nandy jukwaa moja



Wasanii wa kike wapinzani kwenye muziki wa bongo fleva nchini, Zuchu na Nandy, watafanya onyesho la pamoja Oktoba 19 jijini Dar es Salaam wakati wa utoaji wa tuzo ya Muziki wa Tanzania (TMA) mwaka 2024.

Kwa mujibu wa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya tuzo huo, Steven Mosha, wasanii wengine wataotumbuiza pamoja na Alikiba, Marioo, Harmonize, Young Lunya, Yammi, Abigal, Christian Bella, Dulla Makabila na Mzee Yusuph.

Kamati hiyo inashirikiana na Baraza la Michezo la Taifa (BASATA), ambapo wanamuziki na wasanii waliofanya vizuri mwaka jana watatunukiwa tuzo.

Sherehe hizo za utoaji wa tuzo kila mwaka, zitatarajiwa kufanyika kwenye ukumbi wa Super Dome, jijini Dar es Salaam.




## MBOSSO, UWOYA, KUNANI PALE?

WABONGO kama kawaida yao, wameanza kuunganisha 'dot' eti mwanadada Irene Iwoya 'alipomuwishi', Mbosso katika siku yake ya kuzaliwa.

Irene ambaye kwa sasa ameokoka, alimtakia kila la kheri msanii huyo katika siku yake ya kuzaliwa, akimtakiwa maisha marefu na mafanikio zaidi, akimalizia kuwa anampenda sana.

katika mtandao wake wa kijamii wa Instagram, Mbosso alimshukuru kwa upendo wake, akielezea jinsi walivyofurahia siku mbili za mwisho walizotumia huko Arusha.

Sasa bwana Wabongo kama kawaida yake, wakaanza kuunganisha 'dot', baadhi wakaonekana kushangazwa na ukaribu wao kupitia maneno hayo.



## Misso Misondo aibuka tena

Kwa mara nyingine wale wazee wa makoti, wakiwa na Dj Misso Misondo, wameibuka na ngoma moja kali iitwayo, 'Tera Ghata.'

Ngoma hiyo imefyatuliwa jana Ijumaa na imeanza kuwatia wazimu mashabiki kwenye mitandao ya kijamii, hasa Youtube.

Kama kawaida yao wamevaa mikoti yao, suruali pana na mbovu, pekupeku, pamoja na vidumu ambavyo wamevivaa mabegani.

Ni kama vile watu walitaka kuwasahau kutokana na kutotoa ngoma yoyote kwa muda sasa, lakini watu wameshtuka na kujua kumbe wapo.

Kikosi cha wachezaji shoo hao wa kiume na DJ Miso Misondo kilichukua umaarufu mkubwa kuanzia mwaka jana kutokana na mwonekano wao, pamoja nyimbo zao kama,'Tumemfuata DJ', ikiwamo kionjo kilichoteka wengi mtaani cha 'umepigaje wapo?'

## TWISTI 5 KALI ZA WAZEE BONGO

**Na Adam Fungamwango**

MUZIKI una safari ndefu sana. Miaka ya 1950 hadi mwanzoni mwa miaka ya 1970 kulikuwa kuna tofauti za muziki zilizovuma, ikiwamo staili ya 'twisti'.

Muziki huu ulikuwa maarufu sana Ukanda wa Afrika Mashariki, pamoja na nchi kama Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Zambia na Zimbabwe.

Hao ni Daudi Kabaka, Losta Abelo, Edward Masengo, Charles Sonko na dada yake Frida Sonko, Nashil Pichen, Peter Tsosi, John Zenze, Fadhili William na wengine wengi ambao wiki ijayo niwaweka historia zao hapa.

Hawa licha ya kuwa wametoka kwenye nchi mbalimbali na hakuna Mbongo hata mmoja, lakini walikuwa maarufu sana hapa nchini kutokana na nyimbo zao kukubalika kwa kiasi kikubwa. Staili ilipendwa na inapendwa hadi leo kiasi kwamba kwenye sherehe za harusi, wazee huwekewa nyimbo za 'twisti' ili kujikumbusha wakati wa ujana wao.

Ni uchezaji unaleta burudani ya aina yake ya kusugua miguu, huku mwili ukienda chini, upande mmoja, halafu unabadilisha upande mwingine. Wakati mwingine unarusha hata miguu mmoja mmoja wakati wa kubadilisha staili ya uchezaji wa 'twisti'.

Leo tunaangalia ngoma 5 za 'twisti' zilizowachengua mashabiki wa muziki Bongo enzi hizo.

### Tanganyika Twisti-Daudi Kabaka

Ni wimbo ambao Kabaka anamwimbia mpenzi wake Masita kuwa anakwenda safari Tanganyika. ( Tanzania kabla ya Uhuri mwaka 1961).

Inavyoonekana mpenzi wake ana wasiwasi, lakini jamaa anamtuliza na kumwambia hawezi kumpenda msichana mwingine yoyote zaidi ya yeye.

Anamwambia aliwahi kufika huko, akatokea msichana akampenda lakini kila anachofanya anakumkumbuka Masita wake yuko Nairobi, hiyo inaonyesha upendo wake mkubwa kwake na hawezi kumsaliti.

### Angelike-John Zenze

Ni wimbo wa mapenzi, jamaa anamlilia Angelike, mpenzi wake ambaye wamegombana na hitilafiana.

Anamwambia arudi waoane, roho yake kila siku inamsumbua. Anakumbuka mengi walivyokuwa wakifanya wakati wa kilele cha penzi lao, hivyo warudiane na wasahau yaliyopita.

### Msichana wa Elimu-Daudi Kabaka

"Msichana wa sura nzuri ni kitu gani kinachokufanya usiolewe, elimu unayo ya kutosha, hata ng'ambo ukaenda ukarudi.

Msichana wa urembo kama wewe uonyeshe mapenzi kwa vijana, ukileta dharau kwa wanaume utazeeka ukiwa nyumbani kwenu, ona watoto wa nyuma yako, wameolewa wamekuacha ukihangaika."

Haya yote ni maneno yaliyomo kwenye wimbo huo. Unawaasa wanawake hasa wenye elimu kubwa ambao wana tabia ya kuona wao ndiyo kila kitu na kuwadharau baadhi ya wanaume, matokeo yake wanaogopwa kwa kukwepa dharau, hivyo kukosa wapenzi.

### Taxi Driver-Fadhili William

Jamaa anamtaka dereva taxi aendeshe gari kwa haraka kwenda Nakuru akamwone mpenzi wake Anna aliyemwandikia barua afike Jumamosi. Lakini gari lilipofika Naivasha lilipata pancha. Ikawa sasa lazima wachelewe. Alipofika Nakuru alimkuta mpenzi wake amekasirika, ikabidi anamwambie ukweli kuwa halikuwa kosa lake, ila gari lilipata pacha.

### African Twisti-Daudi Kabaka

Huu ni wimbo wa ajabu kidogo. Umetengenezwa enzi ya uduni wa teknolojia, lakini ikawezekana kubadilishwa sauti za binadamu kuwa kama wanaoimba ni wanyama.

"Afrika wote wanapenda twisti, hata sisi wanyama na mwituni tunaipenda na kuimba.

Tucheze tuimbe twist sisi wanyama wa mwituni." Sauti ni kama za vikatuni, lakini zikipangiliwa kwa sauti.

Wanyama hao ni kundi, ambao mmoja aliimba sauti ya kwanza ni Zangu na yule aliyeimba sauti ya tatu na ya pili ni Juma.

FILAMU

## My in Law: Mkwe muuaji

**Na Adam Fungamwango**

FILAMU inaitwa 'My in Law', inayoonyesha baadhi ya matatizo yaliyomo kwenye baadhi ya familia zetu za Kiafrika.

Lakini kwa siku za karibuni tumegundua kuwa baadhi ya matatizo au changamoto tunazoziona kwenye ukoo au familia za Kiafrika zipo pia kwenye tamthilia za Kihindi, Kihispania, Kifilipino na nyinginezo, hivyo kuonyesha baadhi ya mambo hayo yanafanana tu.

Kwenye filamu hii tunamwona mama mmoja mwenye roho mbaya, ya kwa nini, chuki, muongo na kizabizabina.

Mama huyu tangu kijana wake aoe alikuwa akifanya kazi ya kumtesa 'mka mwana' wake licha ya maonyo ya hapa na pale hadi kufikia kusababisha umauti.

Imechezwa na Mama Besenga, Roney, Dora, Chriss, Filipo na wengineo. Kijana Roney anaishi vema na mkewe Dora. Wanapendana kama chanda na pete, na kufuatana kama kumbikumbi. Mama mkwe anaonekana hapendezwi na tabia hiyo. Anaona kama vile mtoto wake amewekewa dawa ya mapenzi, maarufu 'limbwata.'

Kuna siku kijana kamnunulia mkewe maua, akakasirika na kusema mbona yeye tangu amzae hajawahi kuletewa maua. Alichofanya ni kumpora mkewe na kuyachukua yeye.

Binti akavumilia mwisho akachoka na kumwambia mumewe achukue hatua ya kukomesha hali hiyo, vinginevyo anaweza kuondoka.

Kijana akamkanya mama yake juu ya tabia hiyo, lakini mwenye hila hana dawa, akaendelea.

Hata mwanawe akiwa amelala na mkewe, yeye alfajiri dirishani kwenda kumwamsha.

Mama mzazi wa binti huyo akaja kumtembelea. Binti akafunguka madhila yote anayofanyiwa na mama mkwe wake, hadi wakati mwingine kufikia hatua ya kupigwa kama ngoma.


Mama wa binti huyo kumbe naye yuko vizuri, akawapaka kijana huyo mpaka mama yake. Mama mkwe mwenyewe alipoa kama maji ya mtungini kwa timbwili alilofanya mama wa binti huyo.

Mama mkwe akamwambia kijana aondoke nyumbani pale kwani anakaa pamoja na mama yake ndiyo sababu. Akiondoka anaishi vema na mkewe Dora.

Kijana akataka kufanya hivyo kwani kampuni ilimpa nyumba, lakini mama yake aling'ang'ania kuwa kama anaenda kuishi huko na yeye anakwenda, na nyumba hiyo wapangishe.

Bado aliendelea na tabia ya kumtesa Dora. Siku isiyo na jina wakati Dora mjamzito alimfuata ndani na kumwambia ni mvivu hafanyi kazi yoyote zaidi ya kulala, akaanza kumpiga ngumi za tumboni ambayo zilimpeleka chini na kuzirai.

Wakati anafanya kitendo hicho Roney aliwasili nyumbani gafla na kukuta tukio hilo la kinyama. Alichukua bastola na kumtwanga mama yake kichwani naye akaanguka chini. Alipokwenda kuwakagua wote wawili walikuwa wameshakata roho.



BT BURUDANI TELE


# Lopez sasa ana amani

MWIGIZAJI na mwanamuziki mkongwe, Jennifer Lopez, amesema kwa sasa ana amani kuishi peke yake baada ya kukamilika kwa taratibu za talaka na mume wake wa zamani Ben Affleck.

Akizungumza hivi karibuni, Lopez ambaye ameolewa mara nne na kuchumbiwa mara saba amesema hana cha kupoteza na badala yake anasonga mbele kuangalia maisha yake mapya.

"Najisikia salama ninapopungukiwa na utukufu, inanisaidia kukua kwa ubora, kwa sababu ana mipaka yako na nina mipaka yangu. Ninaenda, hapa ndipo salama na amani zaidi," amesema.





## Toke atoa ushauri wa bure

MWIGIZAJI na majasiriamali kutoka Nigeria, Toke Makinwa, amewashauri wanawake kuacha tabia ya kuzungumzia mambo yao binafsi wakiwa na marafiki wao.

Akizungumza na wafuasi wake wanawake katika ukurasa wa Instagram, amesema suala linaloathiri urafiki wa kike ni kushiriki taarifa binafsi kati yao na watu wengine muhimu.

" Mkataba wa rafiki yangu wa karibu ni mimi na wewe, sio wewe pamoja na mtu wako wa maana, inavunja moyo kuona marafiki wengi wa kike haufiki mbali kwa sababu ya kosa hili ambalo wanawake wengi tunafanya." Amesema Makinwa.

## Kanye awaziba midomo wambea

RAPA maarufu kutoka Marekani, Kanye West, hatimaye ameziba midomo ya watu baada ya kuonekana akiwa pamoja na mke wake ambaye ni mwanamitindo na mbunifu wa Australia, Bianca Censori.

Awali, kuliibuka uvumi kwamba wanandoa hao wameachana baada ya kudumu kwa miaka miwili,

Kanye aliamua kuzima uvumi huo baada ya kuonekana hadharani na mkewe wakiwa na furaha zaidi.





## Ini Dima atoa habari njema

BAADA ya kuchukua hatua mbalimbali za kupunguza uvimbe ndani ya tumbo, mwigizaji wa Nollywood Ini Dima-Okojie, hatimaye ametangaza kuwa umepungua.

Mwigizaji huyo alifichua habari hiyo njema kwa wafuasi wake wa TikTok, akisema uchunguzi uliofanyika majuzi umeonyesha kuwa ukubwa wa uvimbe umepungua kwa kiasi kikubwa.


"Nilifanya mabadiliko ya mtindo wa maisha tangu nilipogundua kuwa uvimbe umerudi. Kwa hiyo nilienda hospitali hivi karibuni kufanya uchunguzi wa ultrasound nashukuru kuona unapungua, kwa hiyo tunafanya kitu sawa," amesema.

## Taylor Swift avunja rekodi

MWANAMUZIKI maarufu wa Pop wa Marekani, Taylor Swift, amevunja rekodi mpya baada ya kuwa msanii wa kwanza wa kike kuingia katika orodha ya mabilionea duniani.

Kulingana na ripoti ya jarida la Forbes la mwezi huu, Swift amekuwa na utajiri wa dola bilioni 1.6. Utajiri huo wa kifedha unatokana na kazi zake za muziki hasa ziara yake ya Eras.

Sehemu ya utajiri wake ni pamoja na dola milioni 600 kutokana na mrabaha na utalii, dola nyingine milioni 600 zimetokana na mauzo ya muziki na milioni 125 za mali isiyohamishika.





KANDA KASKAZINI

# Uendeshaji mashauri mahakama ya rufani kidigitali sasa wanukia

**Na Cynthia Mwilolezi,**

ARUSHA

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, ameagiza majaji wa Mahakama ya Rufani na watumishi wote kuwa tayari kufanya kazi kwa kutumia Mfumo wa Usimamizi wa Mashauri ulioboreshwa 'Advanced e-Case Management System' (e-CMS).

Amesema mashauri yaliyoendeshwa kupitia mfumo huo, yameshaiva kwa ajili ya kupokewa Mahakama ya Rufani.

Akizungumza jana jijini hapa wakati wa mkutano wa nusu mwaka wa Mahakama ya Rufani, Profesa Juma alisema ni vizuri majaji na watumishi wa mahakama hiyo kuendelea kufanya mazoezi ya kuutumia mfumo huo.

"Mahakama ya Tanzania inaendelea na jitihada za kuimarisha matumizi ya teknolojia katika mfumo wa utoaji haki. Ngazi za chini za kimahakama zimepiga hatua kubwa katika matumizi ya TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) hususan e-CMS.

"Nafahamu kuwa Msajili wa Mahakama ya Rufani yuko katika hatua ya kupitia kanuni za Mahakama ya Rufani ili kuona kama zinaendana na mifumo ya kielektroniki (e-CMS) ili kusiwe na changamoto za kikanuni katika kushughulikia mashauri ya rufani zinazotoka katika mahakama za chini ambazo zilisikilizwa kwa mfumo wa e-CMS," alisema.

Kutokana na maendeleo hayo, alisema ni dhahiri kuwa wakati wote kuanzia sasa, Mahakama ya Rufani itapokea rufani kwa njia ya mfumo wa e-CMS kutoka mahakama za chini.

Aidha, aliomba Kurugenzi ya TEHAMA iandae mpango mzuri utakaowawezesha majaji na watumishi namna bora ya kuwakumbusha mambo muhimu ya kuendelea kuutumia mfumo wa e-CMS.

"Artificial Intelligence (akili mnemba) inatakiwa kutusaidia kutumia hizi taarifa. Nitumie fursa hii kuwapongeza sana idara ya TEHAMA kwa umahiri, ujuzi na ubunifu wao mkubwa wa kutumia 'artificial intelligence' katika ujenzi wa mifumo ya Kitanzania, ambayo imeiwezesha Mahakama ya Tanzania kuleta ufanisi, uwazi na weledi katika kufanya kazi za utoaji haki," alisema.

Alisema lengo la mkutano huo ni kufanya tathmini na mapitio ya shughuli za Mahakama ya Rufani, kwa lengo la kuangalia walikotoka, walipo na wanakokwenda katika kutekeleza malengo ya mwaka ya Mahakama ya Rufani.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa hadi Juni, mwaka huu, Mahakama ya Rufani ilikuwa na mashauri 1,248 ya mrundikano, yaani yanayozidi miezi 24.

"Idadi hii ya mashauri kwa idadi ya majopo 11 tuliyo nayo ni kusema kuwa kila jopo la majaji watatu wa rufani lilikuwa na mzigo wa mashauri 113. Kwa maana hiyo, kila jopo lingehitaji vikao vitatu kumaliza mashauri hayo. Kwa bahati mbaya sana, mashauri mahakamani ni kama matunda kwenye mti, yanakomaa kila sekunde.

"Kwa hiyo inahitaji mkakati maalum wa kuyaondoa yote na kuhakikisha yale yanayokomaa (backstopping) hayafikii hatua ya hiyo," alisema.

Alisema Mahakama ya Tanzania inaendelea na jitihada za kuimarisha matumizi ya teknolojia katika mfumo wa utoaji haki na ngazi za chini za kimahakama zimepiga hatua kubwa katika matumizi ya TEHAMA hususan e-CMS.



Mkuu wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Zainab Abdallah (kushoto), akijiandikisha kwenye daftari la mkazi katika Ofisi ya Ofisa Mtendaji Kata ya Mbaramo, jana. Kulia ni Kalani wa Uandikishaji, Adeline Magezi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## NHIF yajifagilia kwa kutoa huduma bora

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), unajivunia kuwa na watoa huduma bora za afya kama sehemu ya wadau muhimu katika kufikia azma ya bima ya afya kwa wote.

Meneja wa NHIF Mkoa wa Tanga, Evance Nyangasi, aliyasema hayo juzi katika maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja baada ya kutembelea baadhi ya vituo vya umma na binafsi vilivyosajiliwa kutoa huduma za afya kwa wanufaika wa mfuko huo.

Alisema wameamua kuwatembelea wanachama wao katika vituo hivyo ili kupata mrejesho wa huduma za matibabu zinazotolewa na mfuko, hali ya utoaji wa huduma, kusikiliza kero mbalimbali na kupata maoni ambayo menejimenti ya mfuko itazifanyia maboresho na kuzipatia ufumbuzi hatimaye kuongeza ari ya utoaji huduma bora kwa wateja wa mfuko.

"Kama tunavyoelewa lengo na shabaha ya mfuko ni kutoa huduma bora zaidi na kukidhi matarajio zaidi ya wanachama wetu. Kituo hiki cha Siha ni miongoni mwa vituo 450 vilivyosajiliwa kutoa huduma za matibabu kwa mkoa wa Tanga.

"Tumepeana mrejesho wa huduma na wahudumu wa hapa lakini pia tumeendelea kutoa elimu juu ya huduma bora kwa mteja. Tunaelekea kwenye bima ya afya kwa wote ambayo lengo ni kuona kila Mtanzania anapata huduma bora za afya bila vikwazo," alisema.

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Siha Polyclinic, Dk. Kasanga Bashir, alisema katika maadhimisho hayo wanaendelea kutoa huduma kwa makundi mbalimbali wenye bima na wasiokuwa nazo.

"Lakini kundi kubwa la wagonjwa ambao tumewahudumia kwa muda wote ni wateja walioko chini ya NHIF. Niushukuru mfuko huu kwa ushirikiano wa kutukutanisha na wateja lakini pia kutusimamia katika kuhakikisha ushirikiano huu unaenda vizuri," aliongeza.

Dk. Bashir alibainisha kwamba kufuatia mabadiliko makubwa yaliyofanywa na serikali katika upatikanaji wa huduma za NHIF kumeleta mwitikio mkubwa kwa wananchi jambo ambalo hata wateja wameongezeka kituoni hapo.

# Jafo ataka umakini ukaguzi bidhaa mipakani

**Na Oscar Assenga,** MKINGA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo, ameagiza taasisi tatu za umma kuongeza umakini kwa kuwa na jicho la tatu la ukaguzi wa bidhaa zinazopitishwa katika Kituo cha Forodha cha Horohoro, mpakani mwa Tanzania na Kenya.

Jafo amelitaka Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Wakala wa VipimoTanzania (WMA) na Tume ya Ushindani (FCC) kuhakiki kwa umakini bidhaa zote zinazopitishwa katika mipaka ya Tanzania na nchi jirani.

Akizungumza juzi katika kituo hicho cha forodha, Jafo alisema lengo la serikali ni kuwalinda Watanzania na watumiaji wa mwisho wa bidhaa na kuwezesha watu wote kufanya biashara.

"Hili la 'scanner' tumelichukua na si muda mrefu kupitia Wizara ya Fedha, tutahakikisha inapatikana pamoja nyenzo za kufanyia kazi ikiwamo 'forklift' itakayokuwa ikinyanyua mizigo.

"Lakini niwashukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa kazi kubwa. Serikali itahakikisha mambo yote muhimu yanatekelezwa, lengo kubwa ni kuboresha utoaji huduma.


"Tunataka kuona jinsi gani taasisi za umma zinasaidia kuhakikisha biashara katika eneo hili mizigo inasafirishwa vizuri baina ya Kenya na bidhaa zinazopita lazima zikidhi viwango vilivyowekwa na kuthibitishwa na TBS na WMA na FCC ili kuwalinda Watanzania na walaji (watumiaji) wa mwisho," alisema Waziri Jafo.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, Mariam Ditopile, aliipongeza serikali kwa kazi kubwa ya kuchochea uwekezaji nchini pamoja na kuweka mazingira mazuri kwa wafanyabiashara.

Alisema mazingira hayo mazuri yamewekwa kwa wafanyabiashara ambao tayari wapo kwenye biashara na viwanda ambavyo vinazalisha bidhaa mbalimbali nchini.

"Leo tumepata fursa ya kuja hapa kituo cha Forodha Horohoro kuona namna kituo hicho cha pamoja baina ya Tanzania na Kenya. Sisi kama kamati tunawapongeza kwa kuongeza ukusanyaji wa mapato kwenye kituo hiki," alisema.

# Bendi za dansi, Kibisa zilivyotikisa enzi za Mwalimu Julius Nyerere



Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akipiga ngoma enzi za uhai wake. **PICHA: MAKTABA**

**Na Adam Fungamwango**

"Tumeonewa kiasi cha kutosha. Tumenyonywa kiasi cha kutosha. Unyonge wetu ndio uliosababisha tuonewe, tunyonywe na kupuuzwa. Sasa tunataka Mapinduzi. Mapinduzi ya kuondoa unyonge, ili tusionewe tena na tusipuuzwe tena". Yalikuwa ni baadhi ya maneno ya Rais wa kwanza wa Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akitangaza Azimio la Arusha mwaka 1967, ambaye Jumatatu ijayo anatimiza robo karne, yaani miaka 25 tangu alipofariki nchini Uingereza, 1999, akiwa na miaka 77.

Azimio lilipitishwa kwenye mji wa Arusha (sasa jiji) mwishoni mwa Januari mwaka 1967 na kutangazwa rasmi, Dar es Salaam, Februari 5 mwaka huo huo.

Katika misingi yake ilikusudia kulinda Uhuru wa Taifa, lakini sio tu Tanzania, bali na mataifa ya jirani ambayo kwa wakati ule yalikuwa katika tawala za kikoloni, misingi yake ililala katika ukombozi wa Afrika na Taifa na kufanya kuwa watu wa taifa huru pasi kuingiliwa na mabepari.

**Matumaini yenu Waafrika ni siasa ya Ujamaa. Njama mbinu za hali ya juu kuangusha ujamaa. Ujamaa ni mzuri kwenye kuleta usawa.**

Pili ilikuwa kurudisha mali zote zilizokuwa zinamilikiwa na mashirika binafsi kuwa mali za serikali, maarufu kama mali ya umma zitakazomilikiwa na wakulima na wafanyakazi.

Kwa kutambua umuhimu huo, serikali ilihimiza wananchi kufanya kazi kwa bidii na kuzuia wanyonyaji.

Hapo ndipo nchi ilipoanza kwa kutaifisha mali za mabepari ambazo walikuwa wamejilimbikizia, pia kuanza kuanzishwa makampuni na kujengwa viwanda mbalimbali.

Ndipo vilipokuja viwanda, mashirika na makampuni mengi ambayo mbali na kufanya makubwa, lakini mengi yalimiliki timu za mpira wa miguu, netiboli, ndondi, mpira wa wavu, na hata bendi za muziki wa dansi, kwaya na taarabu.

Vile vile baadhi ya wamiliki hata vikundi ya ngoma za utamaduni ambazo kwa wakati huo vyote vilibatizwa jina la 'Kibisa', kutokana na kundi moja bora kabisa la aina hiyo, lililokuwa likimilikiwa na Shirikika la Maendeleo Dar es Salaam (DDC). Kundi hilo liliitwa DDC Kibisa Ngoma Troupe. Ndipo kwa kufupisha tu mashabiki waliita Kibisa kila kikundi ya utamaduni hata kama kilimilikiwa na kampuni au shiriki lingine.

DDC pia ilimiliki bendi ya muziki ya dansi maarufu hadi leo, DDC Mlimani Park Orchestra, ikiwa na mtindo wake wa Sikinde Ngoma ya Ukae.

Tukirudi kwenye mada halisi, ni kwamba baada ya maneno ya Mwalimu, utekelezaji ukafanyika kama nilivyoanisha kuutaifisha na kuunda Mashirikika na Makampuni mengine, lakini pia watu walihimizwa kufanya kazi kwa bidii, na kuundwa na Vijiji vya Ujamaa.

Kwa kumuunga mkono, wanamuziki wa Tanzania hawakukaa kimya, kwani baada ya Azimio la Arusha walitunga na kuimba nyimbo nyingi sana kuunga mkono na kuwahimiza wananchi kufanya kazi na hata kwenda kujiunga na Vijiji Vya Ujamaa.

Ujamaa ulitamalaki, lakini kuna baadhi walikuwa wakiupiga vita, lakini Mwalimu Nyerere alikaa imara kuueleleza. Kurugenzi Jazz Band ya Arusha, wakatoa wimbo unaitwa 'Ujamaa' wenye maneno yafuatayo.

"Matumaini yenu Waafrika ni siasa ya Ujamaa. Njama mbinu za hali ya juu kuangusha ujamaa. Ujamaa ni mzuri kwenye kuleta usawa. Tutaendelea hatutarudi nyuma. Tulikwishajua matatizo kutashinda. Mawazo sahau ujamaa utakufa. Fungeni vibwebwe tujenge ujamaa." Nchi ilikuwa ya kijamaa kweli kweli.

NUTA Jazz Band, wana Msondo Ngoma, haikubaki nyuma, nayo ilitoa wimbo unaitwa 'Kijiji cha Ujamaa'

"Ndugu zangu, mimi sina kazi, sasa nitapata tabu. Siku nyingi nimefanya bidii, ili niweze kupata kazi, kujitahidi ndiyo nimeiharibu kazi, ndiyo siipati. Sasa nitafanya nini mie, ooo, nakufa.

'Ndugu zangu wamenieleza niende katika kijiji cha ujamaa, nikajiunge na wenzangu, nipate mahitaji yangu, shida ziniondoke. Kwa sasa naondoka, nakwenda zangu, katika Kijiji cha Ujamaa, nimechoka sasa mwenzenu na mambo ya mjini."

Yalianza kufa kwenye miaka ya 1990 baada ya kuanza kushindwa kujiendesha, na yakawa yanaleta hasara.

Kuna sababu nyingi, ikiwemo kuwa na wafanyakazi wengi kuliko uwezo wa kuzalisha.

Mengine yalibinafsishwa na sasa yapo mikononi mwa watu binafsi. Yapo ambapo serikali imeingia ubia na watu binafsi, maarufu kama wawekezaji. Machache sana ndiyo bado yanamilikiwa kwa asilimia mia moja na serikali, mfano Shirikika la Ugavi wa Umeme, TANESCO.

Huo ndiyo ulikuwa mwanzo wa timu za michezo mbalimbali, na bendi kuvunjika, lakini pia hata Siasa ya Ujamaa ndipo ilipoanza kulegalenga.

Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, akipiga ngoma, ikiwa ni ishara ya kuenzi utamaduni wa Kitanzania na Mwafrika kwa ujumla, na ilionekana kipindi chake wakati kulipokuwa na bendi nyingi za dansi zilizokuwa maarufu na zenye nguvu, Pamoja na vikundi ya utamaduni na sanaa, ikiwemo DDC Kibisa Ngoma Troupe.

***Tuma meseji 0716 350534***

## Waliokufa kimbunga Milton wafikia 16

**FLORIDA**, Marekani

IDADI ya watu waliokufa kutokana na kimbunga Milton nchini Marekani imefikia 16, huku eneo kubwa la jimbo la Florida likiwa limeathirika.

Maofisa wa jimbo hilo, walisema jana kuwa idadi hiyo huenda ikaongezeka katika siku zijazo kutokana na kuendelea na kazi ya uokoaji na kutathmini kiwango cha uharibifu.

Idara ya Utekelezaji Sheria ya Florida ilithibitisha idadi hiyo kupitia kituo cha CBS News.

Wakati huo huo, Nasa inakagua kiwango cha uharibifu kwenye Kituo chake cha Anga za Juu cha Kennedy katika eneo la Cape Canaveral, Florida.

"Mara tu upepo ulipotulia hadi kiwango salama, timu zetu za wahandisi zilianza ukaguzi wa awali ili kuhakikisha madaraja ni salama na yanaweza kutumika," Nasa ilisema, na kuongeza kuwa watachunguza kituo chote.

Kimbunga Milton kulichelewesha uzinduzi uliopangwa kufanyika Alhamisi wa chombo sayansi cha Europa Clipper, kitakachorushwa hadi kwenye mwezi wenye barafu wa Jupiter Europa. **BBC**

## Rais Ramaphosa kutoshtakiwa

**CAPETOWN,** Afrika Kusini

RAIS wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa hatakabiliwa na mashtaka kwenye kashfa ya fedha taslimu zilizofichwa kwenye shamba lake yaiyoibuliwa miaka miwili iliyopita na kupelekea kuitishwa kwa uchunguzi maalum wa polisi.

Waendesha mashtaka walisema jana kwamba uamuzi wa kutomshtaki Ramaphosa kwenye kadhia hiyo umechukuliwa baada ya uchunguzi wa kina kufanyika.

Kashfa hiyo iliyopewa jina la "farmgate" ilihusisha tuhuma za kuibiwa kwa dola 580,000 taslimu kwenye nyumba ya shambani ya kiongozi huyo.

Wizi huo uliokuja kubainika na mmoja wa walinzi wake.

Inatajwa kuwa Ramaphosa alikuwaameficha kiwango hicho kikubwa cha fedha kwenye kochi ili kukwepa mamlaka za ukaguzi wa fedha za kigeni.



Upinzani ulitumia hoja hiyo kulitaka bunge kupiga kura ya kutokuwa na imani naye mwishoni mwa mwaka 2022, lakini chama chake, ANC, kilitumia wingi wake bungeni kuzuia mchakato huo. **DW**

# Jaji Mkuu Kenya kuunda jopo kusikiliza kesi ya Gachagua

**NAIROBI,** Kenya

JAJI Mkuu wa Kenya, Martha Koome, ataunda jopo la majaji watakaosikiliza shauri la kumwondoa madarakani Naibu Rais Rigathi Gachagua.

Hatua hiyo inakuja baada ya jaji Lawrence Mugambi, kuwasilisha kesi ya kupinga kutimuliwa kwa Gachagua, akiomba suala hilo lisikilizwe kisheria.

Jaji Mugambi aliwasilisha ombi hilo jana asubuhi katoka ofisi ya jaji mkuu akidai suala hilo linaibua masuala mazito ya kikatiba ambayo yanahitaji kuwapo kwa jopo kusikiliza kwa manufaa ya Wakenya.

Wakati hayo yakijiri, ratiba iliyotayarishwa na Karani wa Bunge la Seneti, inaonyesha kuwa Naibu Rais, Rigathi Gachagua atakuwa mbele ya chombo hicho Oktoba 17, majira ya nne asubuhi kuwasilisha utetezi wake dhidi ya tuhuma zinazomkabili.

Kikao hicho kitadumu hadi majira ya jioni kutoa nafasi ya mahojiano.

Katika kipindi hicho, mawakili wa Gachagua pia watapata fursa ya kuwaita mashahidi kwenye kikao cha seneti ambacho watasaidia kuokoa wadhifa wa kiongozi huyo.

Timu yake ya mawakili ilisema jana kuwa wana mashahidi kadhaa, lakini hawakufichua majina yao.

Baada ya uwasilishaji wake, Maseneta watapata nafasi ya kuhoji na kutafuta ufafanuzi kutoka kwa Gachagua, kabla ya kuutaka upande wa utetezi kutoa mawasilisho ya mwisho.

Timu kutoka Bunge la Kitaifa ambalo lilipiga kura ya kumwondoa madarakani Gachagua, itakuwa na kipindi kama hicho cha kutoa hitimisho la mwisho. Kikao cha kupiga kura kinatarajiwa kuanza mwendo wa saa moja nusu jioni.

Jumatano ijayo, timu ya Bunge la Kitaifa ikiongozwa na mwasilishaji wa hoja hiyo, Mbunge wa Kibwezi Magharibi Mwengi Mutuse, itakuwa na muda kuwasilisha kesi yao ambapo mashahidi kadhaa wataitwa kwenye kikao hicho.

Gavana wa Nairobi Johnson Sakaja, Katibu wa Baraza la Mawaziri, Mercy Wanjau na aliyekuwa Kaimu Ofisa Mkuu Mtendaji wa KEMSA, Andrew Mulwa, wako kwenye orodha ya watu watakaotetea hoja ya kuondolewa madarakani kwa Naibu wa Rais.

Wakati huo huo, Waziri Mkuu wa Haiti, Garry Conille, amewasili nchini Kenya kwa ajili ya kufanya mazungumzo na Rais William Ruto.

Katika mazungumzo hayo, Conille anatarajiwa kumwomba kupeleka askari zaidi wa polisi kusaidia kulinda hali ya utulivu katika taifa hilo lenye machafuko.

Rais Ruto ameahidi kupeleka polisi 1,000 ifikapo Januari mwakani kama sehemu ya misheni ya kimataifa ya kulinda usalama.

Kenya imepeleka kikosi cha polisi 400 nchini Haiti na imeahidi kuongeza 600 ndani ya wiki chache zijazo. **BBC**



Wafanyakazi wa Shirika la Msalaba Mwekundu wakibeba mwili ulioopolewa majini baada ya meli kuzama katika Ziwa Kivu, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) juzi na kuua watu 34. **PICHA: MTANDAO**

## Misri, Somalia, Eritrea zakubaliana kuungana

**ASMARA,** Eritrea

VIONGOZI kutoka mataifa ya Misri, Somalia na Eritrea, wamekutana na kukubaliana kuanzisha ushirikiano mpya wenye nguvu.

Nchi hizo tatu zote zimekuwa na uhusiano mbaya na Ethiopia na hatua hiyo inaashirika kama ujumbe wa onyo.

Katika kikao hicho kilichofanyika katika mji wa Asmara nchini Eritrea, marais Rais Isaias Afwerki, kutoka Misri, Abdul Fattah al-Sisi, na Hassan Sheikh wa Somalia, waliwekeana makubaliano.

Kutoelewana kwa kidiplomasia hivi karibuni kumeifanya Somalia kuwa na uhusiano wa karibu na Misri na Eritrea, ambazo zote zina migogoro ya muda mrefu na Ethiopia.

Waziri wa Habari wa Somalia, Daud Aweis, alisema kuwa mkutano huo ulihusu ushirikiano kati ya nchi hizo tatu.

"Hatujadhamiria kuanzisha chochote dhidi ya Ethiopia" Waziri huo aliiambia Focus on Africa.

Aliongeza "Ethiopia ni jirani yetu tumekuwa tukishirikiana kwa muda mrefu, ingawa baadaye uongozi wao ulikuja na sababu ya kutikisa utulivu katika eneo hilo, lakini mkutano hauna uhusiano wowote na Ethiopia."

Katika picha iliyotolewa na serikali ya Eritrea baada ya mkutano huo, iliwaonyesha viongozi hao wakiwa wameshikana mikono.

Hiyo ni ziara ya kwanza ya sisi nchini Eritrea, wakati rais wa Somalia alikuwa amezuru nchi hiyo mara tatu ndani ya mwaka huu. **BBC**

# Mil.900/- zinahitajika ujenzi jengo maalum la wagonjwa

**Na Ally Hengo, KISARAWE**

HOSPITALI ya Wilaya Kisarawe inahitaji zaidi ya milioni 900 kujenga jengo la wodi ya wagonjwa maalum (VIP), baada ya lile la awali lililojengwa mwaka 1990 kushindwa kumudu idadi ya wagonjwa wanaotakiwa kulazwa.

Jengo la sasa ambalo ni chakavu lina uwezo wa kulaza wagonjwa tisa, idadi ambayo ni ndogo kulingana na upanuzi wa hospitali hiyo hivi karibuni.

Mjumbe wa Kamati ya Utafutaji Fedha za Ujenzi huo, Dk. Hyasinta Lugila, alisema jana kutokana na changamoto hiyo Novemba 2, mwaka huu, watafanya harambee ili kutafuta fedha hizo.

Alisema hospitali hiyo ambayo hupokea wagonjwa kutoka mikoa ya jirani, imekuwa ikikosa huduma kwa baadhi ya wagonjwa wenye uhitaji wa wodi hiyo na kulazimika kuwapeleka wodi za kawaida, wakati walitakiwa wawapo wodi maalum.

Dk. Lugira ambaye ni mtaalamu wa magonjwa ya watoto, alisema uwapo wa hifadhi ya kitalii umechangia hospitali hiyo kupokea wagonjwa wa dharura wanaokwenda kutalii na kutokana na uwezo mdogo wa wodi maalum hiyo, huleta taswira mbaya kwa wageni.

Mganga Mfawidhi hospitalini hapo, Dk. Yona Kabata, aliwaomba wadau na taasisi mbalimbali kujitokeza kuchangia ili kuwezesha hospitali hiyo kuongeza huduma ya maalum kwa wagonjwa wanaofika hapo kutibiwa.

Alisema kwa sasa hospitalini hapo kuna madaktari bingwa tisa, hivyo kufanya huduma kuimarika na mahitaji kuongezeka.

Harambe hiyo ambayo inatarajia kufanyika katika viwanja vya Shule ya Sekondari ya Minaki, mkoani Pwani, mgeni rasmi ni Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemano Jafo.



Ofisa Uhusiano wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Enock Bwigane, akifafanua jambo wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja juzi, Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Vyuo vikuu vina mchango mkubwa utekelezaji haki, usawa kiuchumi'

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imesema vyuo vikuu vina mchango mkubwa katika utekelezaji wa vipaumbele vya haki na usawa wa kiuchumi kupitia Programu ya Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa (GEF).

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Felister Mdemu, aliyasema hayo juzi Dar es Salaam, wakati wa ufunguzi mkutano kuhusu GEF, uliowahusisha makamu wakuu wa vyuo vikuu nchini.

Mkutano huo ulioandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya Wanawake (UN Women) kwa kushirikiana na wizara hiyo, uliohudhuriwa pia na Mshauri wa Rais na Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri ya Taifa GEF, Angellah Kairuki.

Alisema lengo la GEF malengo ni kutimiza azma ya nchi kufikia usawa wa kijinsia miongoni mwa jamii na mwendelezo wa utekelezaji wa Azimio la Ulingo wa Beijing la Mwaka 1995.

"Azimio lilitoa maeneo 12 ya utekelezaji na kila nchi ilipaswa kuchagua maeneo yake ya vipaumbele kwa ajili ya utekelezaji ili kufikia usawa wa kijinsia. Hivyo, Tanzania kama nchi ilichagua maeneo matano ya utekelezaji.

"Maeneo hayo ni uwezeshaji wanawake kiuchumi; kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto; kuongeza ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi na maamuzi; elimu, mafunzo na ajira na uingizaji wa masuala ya jinsia katika sera za kisekta," alisema.

Mdemu alisema kupitia malengo hayo, vyuo vikuu vina mchango mkubwa katika utekelezaji kwa sababu huko ndiko wanakowalea na kuwakuza vijana na pia hizo ni taasisi kitovu cha tafiti mbalimbali ambazo ni muhimu katika kupanga mipango na kuandaa sera jumuishi.

"Naamini kwa ushirikiano wa pamoja tutaweza kutekeleza ahadi za nchi kwenye Jukwaa hilo sambamba na kumwezesha Dk. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Tanzania ambaye ni kinara wa jukwaa hilo kuendelea kung'ara," alisema.

Naibu Mwakilishi wa UN Women Tanzania, Katherine Gifford, alisema: "Tunayo furaha kuwa hapa leo kuzungumza na wasomi wanavyoweza kuendesha, kuainisha ahadi za GEF Tanzania.

"Tunatazamia kubadilishana uzoefu na mitazamo kuhusu jukumu muhimu la vyuo vikuu na taasisi za kitaaluma katika kuendeleza ajenda hii ya kimataifa."

Alisema UN Women inatambua umuhimu wa wasomi katika kushughulikia uwapo wa usawa wa kijinsia akisema zina uwezo wa kushawishi sera, kuunda kanuni za kijamii na kuwaandaa viongozi wajao kwa maarifa na zana za kukuza usawa wa kijinsia.

"Tunaposonga mbele tunahitaji kujenga uhusiano thabiti kati ya wasomi na washikadau katika sekta mbalimbali, ikiwa ni pamoja na serikali na viwanda. Kwa kufanya hivyo, tunaweza kuhakikisha utafiti unaofanyika ndani ya vyuo vikuu, unatafsiriwa duninani kwa usawa wa kijinsia," alisema.

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Dodoma (UDOM), Prof. Wineaster Saria, alisema mkutano huo umeongeza uzoefu katika masuala ya kijinsia hasa kuyazungumzia kuanza ngazi ya chini hadi vyuo vikuu.

"Kazi kubwa niliyoiona na ya msingi ni vyuo vya hapa nchini, kujifunza kutoka kwa wenzetu wa vyuo vya Kenya, kupitia utafiti wao namna wanavyotekeleza masuala haya ili jinsi zote kuwa na fursa sawa," alisema Prof. Saria.

Alisema ili kukuza usawa wa kijinsia malezi yenye mrengo huo ni muhimu kuanzia ngazi ya nyumbani na hatimaye taasisi za elimu ya juu kutilia mkazo masuala hayo.

Profesa Judith Waudo kutoka Chuo Kikuu Nairobi, Kenya, alisema ni wakati wa wanazuoni kufikisha matokeo ya tafiti wanazozifanya kwa umma kwa lugha rahisi kufikisha ujumbe na kuleta matokeo chanya.

"Mara nyingi tunafanya tafiti na kuzifungia hii maana yake tunazungumza wenyewe kwa wenyewe, bila kujali kuhusu wananchi. Tumejitahidi kufikisha ujumbe kwa umma kupitia miradi tunayofanya kutoka chuoni," alisema Prof. Waudo.

## Wapelekwa kukabili ugonjwa wa Mpox

**Na Sabato Kasika**

WAFANYAKAZI 750 wa kujitolea kutoka Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania (TRCS), wamepelekwa katika mikoa inayopakana na nchi jirani kutoa elimu ya kujikinga na mlipuko wa ugonjwa wa nyani (Mpox).

Meneja wa Kukabiliana na Maafa wa chama hicho, Samwel Katambam aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam.

Katamba alisema chama hicho kina wafanyakazi wa kujitolea 50 kila mkoa na kwamba ndio wanaotoa elimu katika maeneo ya mikoa yao iliyo kwenye hatari ya kukumbwa na ugonjwa huo.

„Tuna vikosi kazi vyetu ambavyo ni wafanyakazi wa kujitolea ambao wanashirikiana na watu wa huduma za afya ngazi ya jamii kutoa elimu nyumba kwa nyumba, katika magari, shuleni na kwenye mikusanyiko ya watu ili wajue dalili za ugonjwa," alisema Katamba.

Alitaja baadhi ya mikoa ambayo chama hicho kina wafanyakazi wa kujitolea ambao sasa wanaendelea kutoa elimu kuwa ni Mara, Mwanza, Kagera, Kigoma, Katavi, Rukwa, Mbeya na Songwe.

„Tanzania si kisiwa, imepakana na baadhi ya nchi zenye changamoto ya magonjwa ya mlipuko ukiwamo wa Mpox, hivyo tumepeleka wafanyakazi hao waelimishe wananchi kuhusu ugonjwa huo, madhara yake na jinsi unavyoambukiza ili wawe makini," alisema.

Alisema jukumu lao ni kuhakikisha wananchi wanakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu ugonjwa huo kwa kuwa ndiyo maelekezo waliyopewa na Wizara ya Afya ambayo wanashirikiana nayo katika vita hiyo.

„Utoaji elimu utaendelea hadi Juni, mwakani, kwani ndio mpango kazi wa Wizara ya Afya kisha tathmini itafanyika ili kuona jinsi ambavyo jamii imekuwa na uelewa kuhusu ugonjwa huo," alisema.

Ofisa wa Maafa wa chama hicho, Christa Christian, alisema moja ya TRCS ni kukabiliana na majanga na kwamba mlipuko wa Mpox ni moja ya majanga ambayo ni muhimu kuyakabili. Naye mtaalamu wa saikolojia wa chama hicho, Maudline Tarazo, alisema watu wanapokumbwa na majanga au magonjwa, wengine hukata tamaa, hivyo chama kulazimika kuchukua hatua za kuwarejesha katika hali zao.

„Vilevile, tunawalekeza kila kupiga simu namba 0800750150 iwapo mtu atahisi kuwa na dalili za ugonjwa huo ili hatua zichukuliwe haraka kwani namba hiyo inapigwa bure," alisema Tarazo.

Tarazo alisema chama hicho kimejaa wataalamu wa fani mbalimbali ambazo huzitumia wakati wa majanga mbalimbali, yakiwamo ya ajali, mafuriko, magonjwa na hata ukame na kimbunga.

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri.
Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging.
Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile.
Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosababisha kuwa na tundu kichwani.

# Damu ya Mariamu-34

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

Kazi iliyofuata ni kuanza kufanya uchunguzi ni, magazeti, redio na televisheni gani zinaweza kutumika kuanzisha sakata hilo.

Kilichokuja kubainika ni kwamba tayari Materu na wapambe wake walikuwa wameshapita kwenye vyombo vingi vya habari na kujaribu kuzuia habari yoyote itakayomhusu.

Ilifanikiwa kwa kiasi fulani, lakini baadhi ya waandishi za uchunguzi walipata fununu ya hilo na wakaingia chimbo kuisaka habari hiyo.

Waandishi wa tatu wa magazeti walikutana na Kamal eneo la siri ambalo hata wao hawakujua ni wapi, wakamhoji kuhusu kuhusika kwake kwa mauaji ya mpenzi wake, ndipo alipowahadhithia kila kitu ikiwamo ushahidi unaoonyesha kuwa bosi wake, Materu ndiye aliyehusika kwa mauaji hayo.

Akawapa ushahidi wa maandishi na video ili hata kama akishtaki, basi ajikaange mwenyewe kwenye mafuta yake.

Siku tatu baadaye, kwa msaada wa dokta Shija, waandishi wengine wa habari za mitandao ya kijamii walipelekwa eneo lingine kwa ajili ya mahojiano.

Nao waliambiwa kila kitu, na kupewa ushahidi, ambao wanahabari zote walikuwa wakipewa kopi, hata flashi nazo zikipopiwa na kupestiwa, ili mwenyewe abaki na ushahidi halisi ambao ungeweza kumsaidia kuepuka kesi inayomkabili.


Baada ya kukamilisha zoezi hilo, ahadi ya kulipua bomu ilikuwa ni Jumatatu. Ndiyo siku ya kwanza ya juma. Ndiyo siku ambayo watu wanakuwa na nguvu za kufanya kazi baada ya mapumziko ya wiki.

Wote waliona siku hiyo ndiyo inafaa, hivyo wakaacha kwanza watu wale wikiendi, na Jumatatu wapate kitu cha kushtua. Kitu ambacho kitabadilisha kila kitu. Kitabadilisha mtazamo wa raia na askari polisi juu ya mauaji ya mrembo Mariamu.

**************************************

Wananchi aliamka na mshtuko walipoamka Jumatatu na kusoma baadhi ya magazeti ambayo yaliweka bayana kuwa habari za kiuchunguzi zikionyesha kuwa mauaji wa Mariamu yalifanywa na kigogo mmoja aitwaye Boniphace Materu na si mpenzi wake Kamal kama ilivyoripotiwa awali.

Yakabainisha kuwa yalikuwa ni mauaji yaliyosababishwa na mapenzi, ambapo Materu alimpenda mpenzi wa mfanyakazi wake, Kamal, lakini kwa bahati nzuri au mbaya binti alikataa katakata kumsaliti mpenzi wake.




**Alipofikishwa ilionekana kabisa kuwa ameshafariki dunia pale pale, kilichofanyika sasa ni kutafuta nguo za michezo na kuivisha maiti kabla ya kwenda kuitupa maeneo ya Tabata Kimanga, karibu na nyumbani kwake.**

Magazeti hayo ya siku hiyo yakasema awali aliyetakiwa kuuawa ni Kamal mwenyewe ili iwe rahisi kumpata binti huyo mrembo baada ya kuona suala hilo linashindikana.

Uchunguzi usio shaka wa waandishi hao ulisema Kamal alianza kupokea vitisho kwa watu wasiojulikana aachane na mwanamke huyo ambaye si saizi yake la sivyo angepoteza maisha.

Baada ya Kamal kumwambia mpenzi wake, Mariamu alijua ni nani aliyefanya hivyo, lakini hakumwambia Kamal, badala yake alikwenda kumpa taarifa Materu kuwa iwapo atamuua mpenzi wake, basi na yeye atajiua pia, na akamalizia kumwambia ," labda aichukue maiti yake ili iwe mpenzi wake, lakini si yeye akiwa hai."

Hii ilimkera sana Materu na kuamua sasa kuchukua uamuzi wa kutoa uhai wa Mariamu kwa kumdhalilisha kiasi hicho, wakati yeye ana uwezo wa kipesa, akiwa amemwajiri hata mchumba wake.

Habari zinasema kuwa mazingira yalitengenezwa na Mariamu akauawa. Kwa mujibu wa moja ya sauti na video zikasema Mariamu aliuawa akiwa anatoka mlangoni kwake kwa kupigwa na kitu kizito na mtu ambaye alikuwa amejibanza.

Watu watatu ndiyo waliohusika, dereva, mtu aliyempiga na chuma kichogoni na mwingine ambaye alikuwa wa akiba kufanya chochote kama msaada kwa mwenzake pindi litakapotokea lolote.

Uchunguzi wa waandishi hao wakadai Mariamu baada ya kupigwa pindi alipotoka ndani alianguka na yule jamaa wa akiba alimsaidia mwenzake kumbeba na kumpakiza kwenye gari, wakampeleka moja kwa moja hadi eneo lililopangwa wakiwa na Materu.

Alipofikishwa ilionekana kabisa kuwa ameshafariki dunia pale pale, kilichofanyika sasa ni kutafuta nguo za michezo na kuivisha maiti kabla ya kwenda kuitupa maeneo ya Tabata Kimanga, karibu na nyumbani kwake.

Hii ni baada ya kufahamu nyendo za marehemu kuwa alikuwa na tabia ya kuamka alfajiri na kukimbia jogging, hivyo walitengeneza mazingira ionekane alianguka. Walimtupa kwenye mtaro kando ya barabara.

Kwa bahati nzuri wakati anaondoka alisahau simu yake ya mkononi ndani aliyokuwa anachaji, hivyo baada ya muda mrefu kutopatikana hewani, mpenzi wake alikwenda nyumbani kwake na kuikuta mwenyewe akiwa hayupo. Na hakuonekana hadi kesho yake ambapo ilifahamika kuwa alikuwa amefariki.

Hii inaondoa dhana kuwa alikuwa ameanguka wakati anakimbia jogging alfajiri. Mtu ambaye hakuonekana tangu jana anakimbiaje jogging alfajiri.

Ndiyo maana wananchi na ndugu wa marehemu waliukataa uchunguzi wa kwanza wa madaktari kuwa marehemu alikuwa ameanguka kutokana na kupatwa na ugonjwa wa ghafla wa moyo.

Wananchi wakadai marehemu alikuwa ameuawa na si kweli kama alianguka, kwani tangu alitoweka tangu jana yake.

Waandishi wakaandika kuwa kulikuwa na harufu ya rushwa kwa baadhi ya madaktari kutoka kwa Materu ili kupindisha ukweli na kupoteza ushahidi.

Baada ya kelele nyingi kupigwa, watu wakitaka uchunguzi urudiwe, ndipo Materu sasa aliposhindwa kupenyeza pesa kwa jopo la pili la madaktari waadilifu ambao walitoa taarifa halisi kuwa Mariamu alikuwa ameuawa.

Jopo hili ndiyo lile lililoongozwa na dokta Shija, kaka yake afande Willy, ambaye kwa kiasi kikubwa alimsaidia Kamal kwenye upelelezi.

Habari zikasema kuwa pesa ile sasa ikahamia kwa askari wasio waaminifu ambao kwa kushirikiana na mtoa rushwa, Materu, waliamua kumsaka muuaji feki ili kumbambikia mzigo huo.

Mtu waliomwona ni rahisi kwao na kila mmoja ataamini ni mpenzi wake Kamal, ndipo kwa kushirikiana na baadhi ya waandishi wasio waaminifu, walitengeneza mazingira ya kijana huyo kuonekana muuaji, na hata kuanza kusakwa na polisi.

Wakasema kijana huyo kwa sasa hajulikani alipo kwani anasakwa kwa tuhuma hizo na Jeshi la Polisi, pamoja na genge la Materu kwa ajili ya kummaliza ili kupoteza ushahidi.

Habari hizi zilipotoka nchi ilisisimka. Kila mmoja alirudisha picha nyuma juu ya mauaji ya mrembo Mariam ambayo yalileta tafrani kiasi cha uchunguzi kufanywa mara mbili, mpaka pale kila mmoja alipoamini mpenzi wake alimuua kwa sababu ya kimapenzi.

Leo waandishi wameingia chimbo na kuibuka na uchunguzi kuwa tajiri Materu, ambaye kwa sasa anawania ubunge kwenye moja ya majimbo ya Kilimanjaro ndiyo mhusika mkuu.

***Itaendelea Jumamosi***

# Azam yasaka mechi za kirafiki

**Na Somoe Ng'itu**

UONGOZI wa Azam FC umesema utatumia muda wa mapumziko wa Kalenda ya Kimataifa kucheza mechi za kirafiki ili kujiimarisha zaidi.

Azam FC itasafiri kuwafuata Prisons kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Oktoba 18, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini Mbeya.

Ofisa Habari wa Azam FC, Hasheem Ibwe, alisema kocha wao mkuu, Rachid Toussi, ameomba mechi za kirafiki ili kuwaongezea kasi wachezaji wake ambao hawajaitwa katika timu za taifa.

Ibwe alisema mechi hiyo zitachezwa bila ya mashabiki kwa sababu kocha anataka kuzitumia kama sehemu ya mafunzo kuelekea michezo yao miwili ya ugenini itakayochezwa huko Mbeya.

"Tunaifahamu vizuri sana Prisons, ili kuwashinda lazima tujiimarishe, tunataka kuwafuata tukiamini tutavuna pointi tatu muhimu. Tunataka kushinda nyumbani na ugenini. Tunahitaji kuendelea na kasi ile ile ya ushindi, ingawa tunajua mechi zote hazitakuwa rahisi, „ Ibwe alisema.

Aliongeza wanashukuru wachezaji wao wako katika hali nzuri na kila mmoja anaonyesha ushindani wa kupata namba kwenye kikosi cha kwanza.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Azam yenye pointi 12 iko kwenye nafasi ya tano nyumba ya vinara, Singida Black Stars, Simba, Fountain Gate na mabingwa watetezi, Yanga.

# KAGERA YATIMUA KOCHA, WANNE KUONDOKA BARA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Kagera Sugar imemtimua kocha wake, Paul Nkata, ambaye ni raia wa Uganda baada ya timu hiyo kushindwa kufanya vyema katika michezo yake ya Ligi Kuu Tanzania Bara, imefahamika.

Mbali na kocha huyo, klabu hiyo pia imefikia makubaliano ya kusitisha mkataba na aliyekuwa Kocha Msaidizi, Marwa Chemberi, pamoja na mwalimu wa viungo, Edward Kaziba.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo jana inasema uongozi umeamua kuliondoa benchi la ufundi kutokana na kutoridhishwa na mwenendo wa timu yao.

„Uongozi unawashukuru makocha hao kwa mchango wao ndani ya klabu yetu na inawatakia la kheri katika majukumu mapya," iliandika sehemu ya taarifa hiyo iliyotoka kwenye Idara wa Habari na Mawasiliano.

Klabu hiyo imesema itawajulisha mashabiki wa timu hiyo benchi jipya la ufundi hivi karibuni.

Nkata, aliyedumu kwa miezi miwili tu, alianza kuifundisha timu hiyo mwanzoni mwa msimu, lakini hadi kufikia raundi ya saba, ameonekana kushindwa kukidhi matakwa ya viongozi na mashabiki wa timu hiyo.

Aliiongoza timu hiyo kucheza mechi saba, ikishinda mchezo mmoja, sare moja, ikikubali kufungwa katika michezo mitano, katika msimamo wa ligi hiyo iko kwenye nafasi ya 14.

Kabla hata mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara haujamalizika, tayari jumla ya makocha wanne kati ya 16 hawapo katika timu zao zilizowaajiri katika msimu huu kutokana na kufanya vibaya.

Kocha wa kwanza alikuwa ni David Ouma wa Coastal Union, raia wa Kenya, ambaye alitimuliwa kabla hata ligi haijaanza kwa kile kilichodaiwa kufanya vibaya kwenye mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika halafu akafuatia Msenegal Youssouph Dabo wa Azam FC, na Fikiri Elias wa KenGold ya Mbeya.

Pamoja na hayo, zipo tetesi Kocha Mkuu wa Pamba Jiji, Goran Copunovic, naye amekalia kuti kavu.



Mshambuliaji wa Yanga Princess, Harieth Udong (kulia), akijiandaa kumtoka mchezaji wa Bunda Queens, katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Karume ulioko Musoma mkoani, Mara wiki iliyopita. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

# Fountain yakomalia fiziki kwa wachezaji

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Fountain Gate, Mohamed Muya, amesema atatumia mapumziko ya Kalenda ya Kimataifa, kujikita kuwaongezea utimamu wa mwili wachezaji wake ili wafanye vyema katika michezo inayofuata ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Muya alisema katika michezo saba aliyocheza amegundua baadhi ya wachezaji wake wana upungufu wa utimamu wa mwili kitu ambacho kinasababisha kufanya makosa yanayowaumiza.

Muya alisema ametumia mapumziko hayo ambapo Taifa Stars ilikuwa inakabiliwa na mechi ya ugenini na baadaye nyumbani dhidi ya DR Congo kufanya marekebisho ambao anaamini yatampatia matokeo chanya.

"Nimefurahia sana mapumziko ya Kalenda ya FIFA, yamenisaidia kufanya kazi ya kurudisha fiziki kwa wachezaji ambao hawako fiti, na wanajua wote, pia katika mambo ya kiufundi wanatakiwa mara kwa mara kupata mafunzo.

Mpaka kufikia raundi ya saba ya Ligi Kuu, nimeona matatizo ni yale yale ya baadhi ya wachezaji kutokuwa na utimamu wa mwili, lakini nilishindwa kuyafanyia kazi wakati ligi inaendelea kwa sababu wachezaji watapata ‚fatiki' na kushindwa kufanya vizuri kwenye mechi," alisema kocha huyo.

Aliongeza mbali na timu yake inaongoza kwa kufunga mabao mengi kwenye Ligi Kuu, lakini pia inaongoza kwa kuruhusu mabao wavuni kwake na yote inatokana na tatizo hilo.

Fountain Gate imefunga mabao 14 katika michezo saba iliyocheza na kuruhusu magoli 12 hadi kufikia raundi hiyo.

Akizungumzia mchezo wao unaofuata dhidi ya KMC unaotarajia kupigwa, Oktoba 20, mwaka huu kwenye Uwanja wa Tanzanite Kwaraa ulioko Babati mkoani Manyara, kocha huyo alisema wataingia kwa nguvu zote kama walivyofanya kwenye mechi nyingine zilizotangulia.

"KMC ni timu nzuri, ni timu yenye upinzani, na kwetu sisi huwa hatuidharau timu yoyote ile, ndiyo maana unaona tumefika hapa," Muya alisema.

Timu hiyo inashika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 13 ikiwa imecheza michezo saba.

## ZISIKUPITE

### TRENT AKARIBIA MADRID
REAL Madrid walikuwa na mpango wa kumsajili beki wa England, Trent Alexander-Arnold, mwenye umri wa miaka 25, kwa uhamisho wa bure msimu ujao wakati mkataba wake na Liverpool utakapokamilika, lakini huenda wakamnunua Januari baada ya beki Mhispania, Dani Carvajal (32), kupata jeraha baya la goti. ***(Sport)***

### KONATE KUTUA LIVERPOOL
LIVERPOOL inaendelea na mazungumzo ya mkataba mpya na mabeki wawili muhimu, Jarell Quansah, mwenye umri wa miaka 21 na beki wa Ufaransa, Ibrahima Konate (25). ***(Mirror)***

### POGBA, JUVENTUS KUTETA
PAUL Pogba mwenye umri wa miaka 31, anajadiliana na Juventus kwa lengo la kumaliza msimu wake wa pili na klabu hiyo ya Serie A na kuanza upya baada ya marufuku yake ya kutumia dawa za kusisimua misuli kupunguzwa na Mahakama ya Usuluhishi wa Michezo. ***(Mail)***

### O'NEIL KUBAKIA WOLVES
KLABU ya Wolves haina nia ya kumtimua Kocha, Gary O'Neil, lakini itampa muda wa kubadilisha kikosi chake baada ya kupoteza mara sita katika mechi saba za mwanzo za Ligi Kuu England. ***(Telegraph)***

### MRITHI WA RODRI ASAKWA
KLABU ya Manchester City imetenga pauni milioni 80 kwa usajili wa wachezaji katika dirisha la usajili la Januari baada ya Rodri ya kujeruhiwa. ***(Football Insider)***

### PEREZ KUREJEA ENGLAND
WEST Ham imeonyesha nia ya kumrejesha mshambuliaji wa zamani wa Leicester City na Newcastle United, Ayoze Perez, katika Ligi Kuu England kwa matumaini mchezaji huyo wa Villarreal mwenye umri wa miaka 31 anaweza kuboresha safu yao ya ushambuliaji. ***(Caught Offside)***

### XAVI ATAJWA OLD TRAFFORD
KOCHA wa zamani wa Barcelona, Xavi anapigiwa upatu kuongoza mradi wa kujenga upya kikosi cha Old Trafford iwapo Erik ten Hag ataondoka Manchester United. ***(El Nacional)***

### DAVID AGOMBEWA ULAYA
JARIBIO la Newcastle United kumsajili mshambuliaji wa Lille, Jonathan David, mwenye umri wa miaka 24, limepata pigo baada ya Barcelona kuingia katika ofa ya kumtaka nyota huyo. ***(Shields Gazette)***

### NEWCASTLE, SPURS VITANI
KLABU ya Liverpool imeungana na Newcastle United na Tottenham Hotspur katika mbio za kumsajili kiungo mshambuliaji, Eberechi Eze, mwenye umri wa miaka 26, kutoka Crystal Palace. ***(Football Insider)***

### BARCA YAMFUATILIA SANE
BARCELONA inamfuatilia winga wa Bayern Munich, Leroy Sane, mwenye umri wa miaka 28, ambaye mkataba wake na timu hiyo ya Ujerumani unamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Sport)***

### CHERMONT AGEUKA LULU
KLABU za Ligi Kuu England ikiwamo Arsenal, Wolves, Everton na Chelsea zimekuwa zikimfuatilia beki wa Santos mwenye umri wa miaka 18 kutoka Brazil, Joao Pedro Chermont. ***(Caught Offside)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDINHO AJIUNGA UMILIKI WA GREENVILLE

## ●●●Nyota huyo asema lengo lake ni kusaidia ukuzaji wa vipaji...

**NEW YORK, Marekani**

NYOTA wa Brazil, Ronaldinho amejiunga na kundi la umiliki wa klabu za Ligi ya Soka ya Marekani, Greenville Triumph na Greenville Liberty, timu hizo zilitangaza hapo juzi.

Triumph hucheza katika Ligi Daraja la Kwanza ya wanaume, huku Liberty ikishindana katika Ligi ya Wanawake.

"Msisitizo wa ushindi na uhuru wa Greenville kwenye mchezo wa vijana kupitia timu za akademi ya wavulana na wasichana, na kiwango cha ubora wa ushindani wa timu ya wataalamu," alisema Ronaldinho katika taarifa yake.

"Kwangu mimi na kundi letu, hii ni fursa ya kusaidia ukuaji wa soka katika umri na viwango vyote, na kuwa sehemu ya jumuiya inayothamini uwepo wa kimataifa na mchanganyiko wa kipekee wa tamaduni."

Ronaldinho, ambaye alishinda Kombe la Dunia mwaka 2002 akiwa na Brazil na kutunukiwa tuzo ya Ballon d'Or 2005, inasemekana alitia saini mkataba huo akiwa kwenye soko la Hisa la New York hapo juzi.

Tangazo hilo halikueleza ni dau gani Ronaldinho alitoa katika Kundi la Greenville Pro Soccer.

"Tuna heshima kumkaribisha Ronaldinho katika familia ya Triumph," alisema Mwenyekiti wa Greenville, Joe Erwin.


"Ushawishi wake katika mchezo haulinganishwi, na uwepo wake ndani ya kundi letu la umiliki unazungumza mengi kuhusu mwelekeo tunaoelekea kama klabu."

Kundi hilo lilisema Ronaldinho aliletwa kupitia kwa Wallace Cheves, mwanachama wa kikundi cha umiliki wa GPS, kupitia Shirika la Cheves.

Ronaldinho aliichezea Brazil mechi 97 na kung'ara barani Ulaya akiwa na Barcelona, Paris Saint-Germain na AC Milan.



# Messi alia na uwanja Venezuela



**MATURIN, Venezuela**

LIONEL Messi alilaumu hali ya Uwanja wa Monumental de Maturín baada ya Argentina kuambulia sare ya bao 1-1 dhidi ya Venezuela katika mechi yao ya kufuzu fainali ya Kombe la Dunia iliyochezwa juzi usiku.

Mvua kubwa iliyonyesha huko Maturin, Venezuela iliathiri uwanja kabla ya kuanza, na hivyo kulazimika kuchelewa kabla ya wachezaji kurejea kucheza kwenye uwanja uliokuwa umelowa maji.

Nicolás Otamendi alianza kuifungia Argentina, lakini Salomón Rondón wa Venezuela alisawazisha katika kipindi cha pili huku timu zikimalizana kwa kugawana pointi.

„Ilikuwa ngumu sana, inafanya mechi kuwa mbaya sana,“ alisema Messi akiiambia TyC baada ya mchezo.

„Hatukufanikiwa kukamilisha pasi mbili mfululizo. Kipindi cha pili tulifanya upande wa kulia zaidi, lakini ni vigumu kucheza hivyo.“

Kiungo Rodrigo De Paul alikiri kufadhaika kwa mchezaji mwenzake aliyeshinda Kombe la Dunia baada ya kipenga cha mwisho.

„Katika hali hii, hatukuweza kucheza soka,“ alisema De Paul.

Ingawa kwa sasa Argentina wanaongoza msimamo wa kufuzu kwa Kombe la Dunia kwa ukanda wa CONMEBOL wakiwa na pointi 19 katika michezo tisa, Messi aliondoka akiwa hajafurahishwa na matokeo hayo.

Nahodha huyo wa Argentina alisema hali ya uwanja haikuruhusu timu yake kutekeleza mchezo ambao ulikuwa umepangwa kuchezwa.

„Tulifungwa kwa sababu uwanja haukutusaidia kufanya kile tunachotaka, ilibidi tufanye mchezo mwingine zaidi ya ule ulioandaliwa,“ alisema Messi.

„Lakini tulijiandaa kwa sababu tulipigana, tukashinda vita, tulicheza na makosa ya wapinzani. Hatukuweza kuhatarisha sana kwa kucheza na pasi za nyuma. Kipindi cha kwanza tulipiga pasi mbili nyuma na maji.“

Kocha wa Argentina, Lionel Scaloni alisema baada ya mechi hiyo hafikirii uwanja unafaa kuchezwa kwa mchezo wa kiwango hicho.

# HAALAND AWEKA REKODI NORWAY

**OSLO, Norway**

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Norway na Manchester City, Erling Haaland, amevunja rekodi ya straika wa zamani wa nchi hiyo, Jorgen Juve, kuwa mfungaji bora wa muda wote baada ya kupachika mabao mawili dhidi ya Slovenia kwenye mechi ya Ligi ya Mataifa ya Uefa.

Ilimchukua Haaland dakika saba kusawazisha rekodi iliyodumu kwa karibu karne na kuweka rekodi mpya kwa bao la dakika ya 62, magoli hayo yanamfanya afikishe mabao 34 na kumpita Juve aliyekuwa na magoli 33.

Mshambuliaji huyo kinara wa Manchester city ambaye hivi majuzi alifikisha mabao 100 katika michezo 105 ya klabu hiyo, amefanya hivyo kwa timu ya taifa baada ya kufikisha mabao hayo 34 katika michezo 36 pekee.

Haaland mwenye umri wa miaka 24 alianza kulitumikia taifa hilo mwaka 2019 na tayari amefunga hat-trick tatu dhidi ya Romania, Gibraltar na Kosovo.

# Southgate hataki tena ukocha

**LONDON, England**

KOCHA wa zamani wa timu ya Taifa ya England, Gareth Southgate, ametangaza hatarudi kwenye ukocha licha ya kuwapo kwa taarifa za kuhusishwa na Manchester United.

Southgate aliyeachia ngazi baada ya kupoteza dhidi ya Hispania katika mchezo wa fainali ya michuano ya Euro 2024 iliyotamatika mapema mwaka huu, amekuwa akihusishwa kutua Old Trafford, huku United ikiwa bado haijaweka wazi hatima ya kocha wao, Erik ten Hag, kufuatia mwanzo mbaya wa msimu.

Akizungumza katika mkutano wa umoja wa klabu ulaya unaoendelea jijini Athens nchini Ugiriki, Southgate amejiweka mbali na tetesi hizo na kusema hatakuwa sehemu ya benchi lolote la ufundi kwa mwaka ujao.

“Sitafundisha timu yoyote nina hakika na hilo, nahitaji kujitathmini na kufanya uamuzi sahihi. Unapoachia majukumu makubwa kama niliyokuwa nayo unahitaji kuupa mwili na akili muda zaidi,” alisema kocha huyo.

# STARS: TUNAJIANDAA KULIPA KISASI DHIDI YA DR CONGO

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars), kimerejea nchini salama, Kaimu Kocha Mkuu wa timu hiyo, Hemed Suleiman 'Morocco' amesema wanajiandaa kulipa kisasi katika mechi ya marudiano dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo).

Stars ilikubali kufungwa bao 1-0 na DR Congo katika mechi ya Kundi H ya kusaka tiketi ya kufuzu Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2025) iliyochezwa jijini Kinshasa juzi.

Morocco alisema licha ya kupoteza mchezo huo, bado wana nafasi ya kurekebisha makosa yaliyoonekana katika mechi hiyo na kuvuna ushindi watakaporudiana Jumanne kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

"Mechi ilikuwa hamsini kwa hamsini, yoyote angeweza kushinda, kuna kosa tulifanya tumeruhusu goli, tutarekebisha hali hii, mimi kama mwalimu nimeona kuna matatizo mengi ukiachilia mbali hilo la kuruhusu bao, hayo yameshapita, inabidi tuangalie mbele kwa sababu tunatakiwa kupata ushindi katika mchezo utakaofuata na kulipa kisasi," alisema Morocco.

Kocha huyo alisema bao hilo limetokana na wachezaji wake kupoteza umakini, lakini hana muda wa kukumbuka kilichotokea na siku chache zilizopo atarekebisha mapungufu kabla ya mchezo wa marudiano.

"Tulipoteza umakini tukaruhusu goli, tunarudi kwenye uwanja wa mazoezi kutatua matatizo ambayo yameonekana, kwa kifupi tu narudia, tusahau yaliyopita, hatuna muda, tuna siku chache tu, naamini tutafanya vizuri," Morocco aliongeza.

Alisema sehemu anayoiangalia zaidi kuelekea mchezo unaofuata ni eneo la ushambuliaji na kutengeneza nafasi ili kupata mabao katika mchezo huo na hakuna kingine kinachohitajika zaidi ya ushindi.

"Mimi kama kocha naamini tuna nafasi ya kufuzu AFCON, Watanzania waendelee kutusapoti, tutafanya kila linalowezekana ili tuwafurahishe nyumbani," aliongeza nyota huyo wa zamani wa Stars. Dakika ya 53, straika wa Stars, Clement Mzize, alijifunga akiwa katika jitihada za kuokoa mpira wa kona.

Matokeo hayo yanaifanya DR Congo kufikisha pointi tisa, ikiwa kileleni katika Kundi H ikifuatiwa na Stars yenye pointi nne huku mchezo wa raundi ya tatu kati ya Guinea dhidi ya Ethiopia unatarajiwa kupigwa leo.

# KMKM kileleni Ligi Kuu Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KMKM SC imepaa kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar baada ya kupata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Mwenge katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Annex B juzi.

Kwa matokeo hayo, KMKM imefikisha pointi 13 wakati Mwenge imesalia kwenye nafasi ya 13 ikijikusanyia pointi nne.

Hiki ni kichapo cha pili mfululizo kwa Mwenge SC ambayo mchezo wake uliopita ilichapwa bila huruma mabao 5-0 na Mafunzo.

Licha ya matokeo hayo, Kocha Msaidizi wa Mwenge, Mustafa Hassan, amesema bado timu yake ina nafasi ya kurekebisha makosa yao na kufanya vizuri katika mechi zinazofuata za ligi hiyo ya juu Zanzibar.

Hassan alisema timu yake imeendelea kupata uzoefu wa michezo ya Ligi Kuu Zanzibar na sasa wameanza kupanga mikakati na kutumia mbinu mpya zitakazowabeba.

Aliongeza bado ugeni wa Ligi Kuu kwa baadhi ya wachezaji wake umekuwa ni tatizo linalowasumbua hasa pale wanapocheza na timu kongwe.

"Ninaamini timu itabadilika, hii inatokana na kiwango wanachokionyesha katika michezo waliyocheza hapa Unguja. Ligi bado changa na bado tunayo nafasi ya kufanya vizuri katika michezo iliyobaki, lengo letu ni kuhakikisha tunakusanya pointi 20 katika mzunguko huu," kocha huyo alisema.




Mshambuliaji wa Namungo FC, Meddie Kagere (kulia), akimtoka beki wa timu hiyo katika mazoezi ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union itakayochezwa wiki ijayo jijini Arusha. **PICHA: MTANDAO**

## Fadlu awatisha Yanga SC

INATOKA UK. 24

Kuhusu kukosekana kwa wachezaji waliopo katika timu mbalimbali za mataifa yao, alisema ni tatizo kwa sababu watajiunga kambini siku chache kabla ya mchezo, lakini si tatizo kwao pekee, hata wapinzani wao, Yanga inawahusu.

"Kutokuwa na baadhi ya wachezaji waliokwenda kwenye vikosi vya timu ya taifa kwenye maandalizi ni tatizo, lakini hata wapinzani wetu pia wanapitia changamoto hiyo, lakini nitajaribu kufanya kila kinachowezekana ili wawe katika kiwango bora kwa ajili ya mchezo huo," alisema kocha huyo.

Aliongeza kwa sasa anaendelea kuwafua wachezaji waliobakia, akifanya mazoezi mara mbili kwa siku, asubuhi wakifanya mazoezi ya utimamu wa mwili na jioni wanakwenda uwanjani kwa ajili ya mazoezi ya ufundi.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba yenye pointi 13 iko katika nafasi ya pili nyuma ya vinara Singida Black Stars yenye pointi 16, lakini imecheza mchezo mmoja zaidi.

Mabingwa watetezi, Yanga yenye pointi 12, imecheza mchezo mmoja pungufu ukilinganisha na watani zao na iko katika nafasi ya nne kwenye mzunguko wa ligi hiyo yenye kushirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali.

Tayari homa ya mchezo huo imeshaanza, huku wanachama na mashabiki wa timu hizo hasa za mikoani wakianza kuhamasishana kutoka mikoani kusafiri hadi jijini Dar es Salaam, kwa ajili ya kushuhudia mchezo huo ambao Simba itakuwa mwenyeji.

## Maxi: Hakuna dabi rahisi duniani

INATOKA UK. 24

alisema nyota huyo.

Alikiri msimu huu Ligi Kuu imekuwa ngumu zaidi kuliko msimu uliopita kutokana na timu nyingi kusajili wachezaji wazuri na kufanya maandalizi bora.

Maxi aliweka wazi anavutiwa na viungo Awesu Awesu wa Simba, Mudathir Yahaya wa Yanga na Feisal Salum wa Azam FC.

Wakati huo huo, wachezaji wa timu hiyo wamekuwa wakifanya zaidi mazoezi ya utimamu wa mwili kuelekea mechi hiyo ya dabi.

Inaelezwa Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi, amekuwa akisisitiza mazoezi ya ‚gym' ili wachezaji wawe na fiziki zaidi kwa sababu anaamini mchezo huo utakuwa na matumizi ‚makubwa' ya nguvu kwa nyakati fulani.

Mkongomani huyo tayari amepachika mabao katika dabi mbili ambazo amecheza, akianza Agosti 9, mwaka huu alifunga bao pekee kwenye mchezo huo, huku msimu uliopita, Novemba 5, mwaka jana, akifunga mabao mawili, akiiwezesha timu yake kuibamiza bila huruma, Simba mabao 5-1.

Mabao mengine katika mchezo huo wa msimu uliopita yalifungwa na Kennedy Musonda, Pacome Zouzoua na Stephane Aziz Ki.

# Michezo

Nipashe

Jumamosi Oktoba 12, 2024


## Messi alia na uwanja Venezuela

UKURASA 22







Fadlu

Maxi

# Fadlu awatisha Yanga SC

### ●●● Kocha huyo atamba wataingia dimbani na nguvu mpya kwa lengo...

**Na Adam Fungamwango**

ILI kuhakikisha inapata ushindi katika mechi ya dabi, Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amesema timu yake haitacheza kama ilivyokuwa kwenye mechi ya Ngao ya Jamii kwa sababu kikosi chake kwa sasa kimeimarika zaidi.

Simba ilifungwa bao 1-0 na Yanga katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya Ngao ya Jamii iliyochezwa Agosti 9, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Wekundu wa Msimbazi watakuwa wenyeji katika mechi ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Oktoba 19, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Akizungumza jijini jana, Fadlu alisema katika mchezo uliopita timu yake ilipoteza kwa sababu ilikuwa na wachezaji wengi wapya, dabi yao ya kwanza na ndiyo walikuwa wamekutana huku wakiwa hawajazoeana.

Fadlu alisema mechi hiyo ya dabi iliyopita imewasaidia baadhi ya wachezaji wake ‚vijana‘ kujua mazingira na matakwa ya mchezo huo, hivyo anaamini mchezo unaokuja wapinzani wao watarajie kukutana na ‚kitu‘ tofauti.

“Nafikiri mchezo wetu wa kwanza Ngao ya Jamii ulitusaidia sana, baadhi ya wachezaji wetu walikuwa ni mara ya kwanza kucheza dabi ya Tanzania, nadhani kwa sasa wameanza kuelewa nini maana ya michezo hiyo.

Sidhani kama tunaweza kuingia tena kama vile, wachezaji vijana tayari watakuwa na uzoefu na wataongeza umakini wakishirikiana na nyota wazoefu waliowakuta, wapinzani wetu watarajie kukutana na aina nyingine kabisa ya mchezo pamoja na umakini wa wachezaji wangu tofauti na mechi iliyopita,“ alisema Fadlu.

Kocha huyo alisema katika mchezo huo hawaendi kulipiza kisasi cha kufungwa mchezo wa kwanza, badala yake wanakwenda kuendelea kupata uzoefu pamoja na kushinda mchezo huo ili kuvuna pointi tatu.

“Hatutaingia kwa kulipiza kisasi, ila kuendelea kupata uzoefu na kushinda kwa ajili ya kupata pointi tatu za Ligi Kuu Tanzania Bara, najua haitakuwa rahisi, lakini tumejiandaa na ugumu ambao tutakutana nao,“ Fadlu alisema.

INAENDELEA UK. 23

# Maxi: Hakuna dabi rahisi duniani

**Na Adam Fungamwango**

KUELEKEA katika mechi ya watani wa jadi itakayochezwa Oktoba 19, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, kiungo mshambuliaji wa Yanga, Maxi Nzengeli, amesema hakuna dabi rahisi duniani.

Akizungumza jijini jana, Maxi, ambaye ni raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, (DR Congo), amesema mechi yoyote ikishaitwa dabi, ambayo inazikutanisha timu zenye upinzani wa asili huwa ni ngumu bila kujali yupi yuko katika kiwango kizuri kwa wakati huo.

Nyota huyo amesema mechi hiyo haitakuwa rahisi kama baadhi ya watu wanavyodhani, ila kama kupata ushindi kwa upande wao itatokana na uwezo, ufundi, mbinu za makocha wao, pamoja na kujituma.

“Anayesema mchezo huu utakuwa rahisi sijui anafikiria nini, kwangu ni mechi ngumu sana, kwa sababu dabi yoyote duniani huwa ngumu na haitabiriki, ndiyo maana unaona tupo mazoezini, tunafanya mazoezi kwa juhudi na bidii kwa sababu ya kwenda kucheza mchezo huo, kama hata mechi za kawaida tu watu tunafanya mazoezi, iweje leo mtu aseme eti dabi si ngumu, au hata atokee mchezaji aseme eti itakuwa ni kawaida tu, hapana,“ alisema Maxi.

Mchezaji huyo ambaye ana msimu wa pili katika kikosi hicho alisema kutokana na kujua siku zote dabi huwa ngumu, ndiyo maana tunahakikisha tunapambana ili kufunga mabao.

Aliongeza wanaendelea kujiandaa vizuri na mchezo huo ili kuhakikisha wanashinda mchezo huo.

“Mchezo utakuwa mgumu lakini kwetu ni muhimu kushinda, mimi nimejiandaa vizuri zaidi ya kawaida, nakumbuka mechi zangu mbili za dabi nimefunga,“

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >